

MALKIA WA KUSINI



Asanteni. Mungu akubariki, Ndugu Don.

² Mwaweza kuketi. Ni kama tu ndio kwanza nifike hapa, sasa inasema usiku wa mwisho. Vema, huu umekuwa mkutano usio wa kawaida kuliko yote ambayo nimekuwa nayo kwa muda mrefu.

³ Wewe ni Ndugu Babbs, sivyo? Nilikutambua leo huko nje mahali tulipokuwa tukila, na tulipomaliza, ni—nilikuwa nikiangalia kule, nikasema, “Hao si ni marafiki zangu kutoka El Dorado?” Nafikiri hiyo ni kweli. El Dorado?

⁴ Naye Ndugu Jack akasema, “Hakika ndio.” Nasi tukaanza kuzungumza pale, halafu basi, muda si muda wajua, ulikuwa umeondoka, sikuweza kukupa mkono. Mungu akubariki.

⁵ [Ndugu Babbs anasema, “Ndugu Branham, ulihitaji chakula na kupumzika, sio kusumbuliwa na sisi.”—Mh.] Loo. [“Tulishuka kuja kuhudumiwa, na tumehudumiwa.”] Asante, ndugu, asante. Ndugu Babbs kutoka El Dorado, ndugu fulani Mbaptisti... [Ndugu Babbs anazungumza tena.] Naam. Naam, bwana, ndivyo. [Ndugu Babbs anaendelea kuzungumza. Sehemu tupu kwenye kanda.]... vizuri hivyo?

⁶ Nami ninaamini una binti wawili wa kupendeza. Nami ninakumbuka mmoja wao alianza, siku moja, kuja jukwaani, naye alikuwa ameolewa kwa muda mrefu, wala hakuwa na watoto wowote. Ndipo alipoanza kuja jukwaani, Roho Mtakatifu akanigeuza, na kusema, “Unatafuta mtoto, basi BWANA ASEMA HIVI, utampata.”

⁷ Nilikuwa huko saa chache tu kabla hajazaliwa, na huyo hapo, alikuwa naye. Mtu fulani aliniambia ana watatu sasa. Ajabu! Hiyo ni... Yeye hutoa kipimo kizuri kila mara, mwajua. Naam. Hilo ni zuri sana. Vema, hilo ni sawa kabisa. Nina furaha sana kwa ajili ya hilo. Nina ninii...

⁸ Ninaamini ya kwamba hiyo ni Biblia. Mwanamke ambaye ana heshima ya kutosha kumlea mtoto katika siku hizi, wakati wanafanya kila kitu kingine na kujaribu kuwaangamiza, mimi... Mungu ataheshimu hilo.

⁹ Nina mama mmoja huko Canada ambaye alikuwa, ninaamini ana umri wa miaka hamsini na mitatu ama hamsini na minne, alikuwa ameolewa tangu alipokuwa na umri wa kama miaka kumi na minane, hawakuwa na watoto, ndipo usiku mmoja, ilikuwa ni wakati Ndugu Jack alipokuwa pamoja nami, ndipo huyo mama akaja, wao ni Wajerumani, ninasahau jina lao sasa hivi, naye akasema... akaja jukwaani, Roho Mtakatifu akasema, “Unatafuta mtoto.”

“Naam.” Akapita huo umri, alikuwa na yapata arobaini na *kitu*, arobaini na nane, arobaini na saba, arobaini na nane wakati huo. Kasema, “Hiyo ni kweli.”

Kasema, “Vema, utamkumbatia mwana, BWANA ASEMA HIVI.”

¹⁰ Sasa, daima angalieni hilo, mnaona, BWANA ASEMA HIVI. Moja ni ono, hilo ndilo ninaloona, basi kile ninachoona Yeye anafanya, hilo ni jambo moja ninasema ninaloangalia, jambo lingine ninasema yale atakayofanya, mnaona. *Hivi* ndivyo ninavyosema, *hivyo* ndivyo anavyosema Yeye, mnaona.

¹¹ Yapata miaka miwili au mitatu ikapita wala hakuna kitu kilichotukia, akawaza, “Vema, kuna kasoro.” Ndipo akaanza kushuku, akasema, “Vema, Ndugu Branham hakuona tu hilo ono vizuri.” Loo, naam.

¹² Kwa hiyo, akasema, baada ya miaka mitatu au minne kupita, basi akasema, “Ninajua siwezi kumpata sasa.” Alikuwa amefikia umri wa karibu miaka hamsini, ama zaidi.

¹³ Na kwa hiyo yeye... Ndipo nikapitia huko kutoka juu, juu, na huko juu kabisa kaskazini, huko Yukon kwenye ziara ya mawindoni, nikapitia huko, na kufanya mkutano wa usiku mmoja katika vijiji vidogo nikipita. Nilipofika kwenye mji huu anamoishi, mbona, mimi, Calgary, nami... Alikuwa... mumewe akaja mkutanoni, yeye hakuja.

¹⁴ Nami nikasema, “Yuko wapi dada?” Nami sikuwa na kabuti, naye akanipa, alitaka kunipa lake, nami nisingelichukua. Naye alikuwa amesimama nyuma, nikasema, “Yuko wapi dada?”

Kasema, “Ndugu Branham, amelemewa na TB.”

Nami nikasema, “Loo, jamani!”

¹⁵ Nami nikasimama na kumwangelia, na kwa namna fulani tu... Huna budi kuhisi hisia za watu. Kamwe huwezi kumsaidia mtu yeyote, isipokuwa uingie ndani yake moja kwa moja pamoja nao, hu—huna budi kuingia katika mateso yao, usipofanya hivyo, unaninii tu, uko nje kabisa. Huna budi kuwa na upendo na kitu fulani kinachokufanya uwe tu moja kwa moja nao.

¹⁶ Basi hilo likaniumiza sana kusikia kwamba alikuwa na kifua kikuu. Nikaangalia, nikasema, “Hiki hapa kilichousababisha: Yeye alitilia shaka kuhusu mtoto huyo mchanga.”

Akasema, “Ndugu Branham, hiyo ni kweli kabisa.”

Nikasema, “Sasa ameenda kombo katika namna fulani ya *itikadi* kuhusu kunywa juisi, na vitu kama hivyo, hali nyama yoyote, wala haninii...”

Akasema, “Hiyo ni kweli kabisa.”

¹⁷ Nikasema, “Hilo ndilo lililomfinyilia chini katika ugonjwa wa TB, mwili wake hauna chakula cha kutosha.” Nikasema, “Nenda ukamwambie ya kwamba nilisema, ‘BWANA ASEMA

HIVI: Usitilie shaka hilo.' Sijali kama ana umri wa miaka tisini, bado atampata huyo mtoto." Mnaona?

¹⁸ Na kwa hiyo akarudi na kumwambia. Ndipo akatupilia mbali juisi zake na kuanza kula kawaida, kisha akarudi, na kuamini jambo hilo. Halafu nilikuwa pamoja na Ndugu Fred Sothmann, yeye yupo hapa mahali fulani. Tulikuwa... Fred, hao watu waliitwa nani? [Ndugu Sothmann anasema, "Dobble. Dobble."—Mh.] Dobble, nasi tulikuwa, mahali hapo palikuwa wapi, huko juu kabisa mwishoni mwa ulimwengu? ["Prince Albert."] Prince Albert, huko Prince Albert.

¹⁹ Naye mwanamke huyu alikuwa mzee hivyo na alikuwa anaenda kumpata mtoto huyu, nao madaktari walikuwa wakishangaa ni kitu gani kingetukia, hakufikiri angeweza kumpata. Kwa hiyo kuonyesha uaminifu wao, na mawazo yao, walimpandisha kwenye gari moshi kama gari la kuchukulia wagonjwa, na kumleta kwenye mkutano huo kuona kile Bwana angesema. Bwana akanena na kusema, "Mwambie, arudi, ana mvulana anayekuja."

²⁰ Vema, mara alipofika nyumbani akamzaa mvulana huyo mzuri, mkubwa, naye huyo hapo. Naye yuko, yeye yuko katika umri wa miaka hamsini na kitu, mnaona. Lakini Yeye hajawahi kushindwa, anaposema jambo lolote, litakuwa hivyo tu, halina budi kuwa.

²¹ Nilikuwa nikiwazia, hivi Ndugu Welch Evans yuko hapa? Ndugu Fred, alikuja? [Ndugu Sothmann anasema, "La."—Mh.] Hakuja kamwe. Nilikuwa nikiwazia, hapa si muda mrefu uliopita, kuwaonyesha tu jinsi ilivyo rahisi, jinsi Bwana alivyo na upendo, na jinsi—jinsi anavyopenda kuponya, yeye... tulikuwa tukivua samaki huko Florida, tulikuwa na mkutano huko Georgia, tukashuka kwenda Florida kuvua samaki kwa yapata siku mbili.

²² Naye huyu Bw. Evans ni Mkristo hodari, ndugu mpendwa; naye ndugu yake si Mkristo, kwa hiyo, alikuwa na duka la chambo. Tilitoka tukaenda katika namna fulani ya msitu kule ambako ilikubidi kuwafukuza nyoka, na mamba tupate kuingia mahali ambapo tungeweza kuvua samaki. Naye ndugu yake alikuwa ameumwa na nyoka-mchacharisha wa ardhini. Sijui, sidhani mnaye huku Louisiana, wao ni maskini wahuni wadogo. Nao ni wabaya sana, wanapokuuma, wanakuua, na kwa hiyo, wao ni wabaya kuliko nyoka wa majini.

²³ Na kwa hiyo, mvulana huyu alikuwa ameumwa na mmoja huko nje, yeye ni mvuvi hodari, nao walikuwa wamempeleka hospitalini. Na yapata miezi mitatu, naamini, sivyo, Ndugu Fred, alikuwa amelazwa hospitalini? Wakati huo alikuwa, gango kubwa mno chini ya mguu wake akitembea huku na huku, walidhani angepoteza mguu wake kama hakupoteza maisha yake, na ilikuwa mbaya sana.

²⁴ Vema, mimi, Bwana alikuwa amenibariki, nami nilikuwa nimeshika, loo, samaki besi, wakubwa mno, nami, nilifurahia sana jambo hilo. Na nilikuwa na mmoja mkubwa kwenye ndoana wala hata nisingeweza kumshikilia. Naye angeninii tu, angeruka, na ilikubidi umwinue juu kwenye ufito wa kuvulia, naye angeitikisa chambo itoke kinywani mwake, nami ningemrushia maskini kishikizo hicho tena, naye akakipata mara ya tatu. Vema, kila mtu akatupa chini ufito wake, akakimbia huko. Na—nami nikasema, “Kamwe siwezi kumshikilia.”

²⁵ Kwa hiyo nikamwacha apumzike kidogo kisha nikajaribu tena. Nami... Mwingine, ambaye angekuwa na uzito wa ratili kumi na mbili, kumi na nne, naye huyu alionekana kama ni wa ratili kumi, ama kumi na moja, nami nilikuwa nimemshikilia, nikasema, “Huyo siye.”

²⁶ Lakini nilipomchosha, nilipokuwa nikimleta ufukoni, Ndugu Evans pale huku amekunja miguu ya suruali yake, wala haogopi chochote, na kwa hiyo, akasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Branham,” pedi nyingi sana na kadhalika, kasema, “Nitakutolea huyo.”

Nami nikasema, “Vema, hilo ni sawa.” Nikasema, “Nitamkokota tu ndani, kama akichomoka hatujali.”

Kwa hiyo akasema, “Nitamshika.”

²⁷ Akaingia tu ndani, na yapata wakati huo maskini mchacharisha wa ardhini, alikuwa amelala chini ya moja ya hizo pedi, akamshika moja kwa moja mguuni. Sijawahi kusikia mwanamume akipiga mayowe *hivyo* maishani mwangu. Ndipo aliporuka kutoka majini, na kuushika mguu wake, na kuanguka ufukoni namna *hiyo*, loo, inakupoozesha tu kwa dakika moja, nikaushika mguu wake, nikaangalia, palikuwa na matundu mawili yaliyoachana tu kwa inchi moja, nayo damu ikitoka kwayo. Nikainyakua bunduki yangu, na kumtafuta yule mchacharisha, nami nikamwona akipitia kwenye magugu namna *hiyo*, hata nisingeweza kumpiga risasi, alikuwa ametoweka.

²⁸ Ndipo nikawaza, “Loo, jamani!” Wala hakuna mtu aliyekuwa pamoja nami wakati huo, kwa kuwa... lakini... ambaye angeweza kunisaidia, maskini Billy Paul alikuwepo. Basi ingenibidi kumbeba mgongoni mwangu kwa yapata maili mbili kupitia kwenye hivyo vijisitu, na ni maji tu, na juu, karibu, wakati mwingine karibu yamefika kwenye goti, naye ana uzito wa kama, karibu mia mbili, kwa hiyo nilijua kingekuwa kibarua kigumu kumvuta kupitia humo.

Kwa hiyo nikawaza, “Tufanyeje?”

²⁹ Naye alikuwa tu akisaga meno yake, akizuia pumzi yake akifanya, “*Sweet! Whiu! Sweet!*” Huku machozi yakitiririka shavuni mwake, ndipo akasema, “Ndugu Branham, mguu wangu

umepooza.” Huenda moja kwa moja kwenye mfupa, mwajua. Kisha kasema—kasema, “Mguu wangu umepooza.” Akishikilia tu meno yake namna *hiyo*. Kasema, “Nahisi ni kama mwili wote umeganda.”

Nami nikawaza, “Loo, rehema! Nifanye nini?”

³⁰ Na mara nikasikia Maandiko hayo, “Watakanyaga vichwa vya nyoka na nge, hakuna kitu kitakachowadhuru.”

³¹ Kwa hiyo, nilivua tu kofia yangu, nami nikasema, “Sasa, jaribu kutulia uwezavyo, Ndugu Welch, ili niweze kushikilia mkono wangu juu ya mng’ato huu.” Naye Baba wa Mbinguni anajua ni kweli.

³² Ndipo nilipoweka mkono wangu juu ya mguu wake pale, na, nikasema, “Baba, Wewe ni Msaada upatikanao wakati wa shida, wala hutupungukii kamwe. Naye ndugu yetu ameumwa na huyu nyoka, na imeandikwa katika Neno Lako ya kwamba watakanyaga vichwa vya nyoka na nge, wala hakuna kitu kitakachowadhuru, nalo linasema, ‘Wakishika nyoka, haitawadhuru.’ Alikuwa akijaribu kunisaidia, ndipo huyu nyoka mwovu akamshika. Sasa, Wewe ni Bwana, Yesu kwenye ukingo huu, hapa tukivua samaki, kama hukuwapo, nisingeenda kuvua samaki, nami ninajua Wewe upo hapa. Nami nakuomba uturehemu, na—na umwondolee sumu hii ya nyoka mguuni mwake.”

³³ Ndipo nikaacha kuomba, wala sikumsikia akiteseka tena. Basi nilipomaliza kuomba, alikuwa ameketi pale akicheka, naye akasema, “Ndugu Branham, sina maumivu.” Kasema, “Yote yamekwisha.” Ndipo akasimama na kutembea huku na huku.

³⁴ Yapata saa tano jioni hiyo, nilikuwa nimeshika samaki besi kumi na mmoja ambao walikuwa na uzito, kwa wastani, karibu, ratili kumi na mbili kila mmoja, nami—nami nikawaingiza ndani, nao walikuwa wakija huku wakiwapiga picha kwenye ua wa watalii huko. Ndipo ndugu yake akaja, kwa hiyo tukaanza kushuhudia jambo hilo. Naye ndugu yake, mwenye dhambi, akasema... alikuwa hospitalini, mnaona. Ni vizuri kuwa Mkristo. Mnaona? “Waaminio watakanyaga vichwa vya nge na nyoka,” haikusema lolote kuhusu asiyeamini. Mnaona? Lakini mtu huyu alikuwa ni mwaminio.

³⁵ Ndipo ndugu yake akasema, naye akamwonyesha mahali pale ambapo... akasema, “Sasa angalia, ndugu, ni vizuri kuwa wa kidini, bali si vizuri kuwa mwendawazimu.” Akasema, “Afadhali uende hospitalini haraka uwezavyo,” kasema, “ukachanjwe, kwa sababu usipochanjwa,” akasema, “huenda ukalemazwa maishani mwako mwote, na unaweza kufa wakati wowote.”

³⁶ Akasema, “Hilo lilitukia asubuhi ya leo yapata saa nne, na hii ni saa tano usiku wa leo, kama chanjo aliyonipa Mungu asubuhi ya leo kukomesha maumivu imedumu kwa muda mrefu

hivi, itaendelea kunidumisha.” Kwa hiyo, ilikuwa... Kwa hiyo, ingali inashikilia, hiyo imekuwa ni miezi, na miezi, na miezi iliyopita, hakuna matokeo mabaya. Kuonyesha tu kwamba Yeye angali ni Bwana Mungu, wa ajabu sana.

³⁷ Ninajua jambo hili, ninachukua muda, wala hatutaki kukaa muda mrefu sana usiku wa leo, nitazungumza tu kwa dakika chache. Lakini nina haja moja zaidi ambayo ningetaka kuomba. Jambo moja, kabla sijaomba haja hii maalum sana, itakuwa, labda, mwaka huu ujao nitakuwa ng’ambo sana, Bwana akipenda, kwa kuwa ninajisikia ya kwamba kama kuna mwaka huu, nami niishi kuuona mwaka huu ujao, nitakuwa nikiiandaa ratiba yangu ya safari sasa hivi. Nalo juma la Krismasi ndio wakati tunapoombea haja zote na kuona mahali ambapo Bwana atatuongoza. Na labda nitakuwa mbele ya wachawi, na kadhalika, kama kawaida, tutakapoenda ng’ambo. Naweza kuwaomba mniombee? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

³⁸ Ninataka kusema ya kwamba huu umekuwa mmoja wa mikutano bora sana ambayo nimewahi kuwamo. Jambo la ajabu sana lilitukia. Ninawapenda watu huko Shreveport, mimi ni mchungaji mwenzena, mwajua. Lakini sikuwa nimewahi kuwa hapa kwa yapata miaka mitano, na nikiendelea tu upesi nilivyoweza kwenda, mchana na usiku. Na yapata miezi miwili iliyopita nilianza, Shreveport ikaingia moyoni mwangu, nami hata nisingeweza kupumzika mchana na usiku. Na hata ikaendelea hata siku moja nilipokuwa nimeketi pale nikiwazia sana juu yake, nikaanza kulia.

Meda akasema, “Kwani kuna nini?”

Nikasema, “Nina hamu sana ya kuona Shreveport.”

Akasema, “Vema, kuna nini?”

Nami nikasema, “Meda, labda kuna tatizo huko chini. Unafikiri tunapaswa kupiga simu?”

³⁹ Na, “Loo,” akasema, “Kama lipo, nafikiri kama—kama likiwapo, wangekupigia simu, Bill.” Kasema, “Unajua jinsi Bwana daima amekuonyesha, wakati Dada Moore alipokuwa anakufa, nawe ulikuwa ukienda zako kule, na jinsi ulivyotoka na kuomba, na mambo mbalimbali, na jinsi ambavyo Yeye amefanya mambo.” Kasema, “Je, amekuonyesha chochote?”

Nikasema, “La.”

⁴⁰ “Vema,” kasema, “kama kuna jambo lolote lililotukia, wangekupigia simu.” Kasema, “Ukiendelea kupiga simu namna hiyo, huenda ikawafadhaisha na kufikiri ya kwamba jambo fulani linaenda kutukia.” Kwa hiyo, kasema, “Kwa nini usiachane tu nayo?”

Nikasema, “Vema, siwezi kabisa kujizuia kuomba, kwa namna fulani. Ninakuwa mpweke sana.”

⁴¹ Ndipo nikakutana na Ndugu Jack, naye akasema, “Vema, tunajisikia upweke kukuona.” Muda si muda mwajua, Dada Moore alikuwa ameinamisha uso wake kwa muda mrefu, akiomba, naye Mungu alikuwa amemwonyesha mkutano huu ujao.

⁴² Halafu tayari nilikuwa nimefanya mipango na baadhi ya Wabaptisti wa—wakati huo. Basi ninii, wakati Ndugu Moore aliposema ilikuwa ni wakati huu, nilishuka nikaenda na kuwauliza. Na ni mchungaji, ama, kanisa, ambalo nilikuwa nikilichunga huko Milltown, Indiana, Kanisa la Kibatisti la Milltown. Hakika hawataki kamwe kuachilia jambo hilo la kila mwaka kwenye Sikukuu ya Kutoa Shukrani. Lakini nikasema, “Ndugu, Bwana ananielekeza Shreveport. Kwa nini, sijui, lakini sina budi kwenda Shreveport.”

Wakasema, “Vema, kama ndivyo ilivyo, endelea, na Bwana awe pamoja nawe.”

⁴³ Hakika nina furaha kwamba nilikuja, limekuwa ni jambo zuri sana kwangu, jinsi Bwana amebariki kila usiku, na amefanya mambo makuu.

⁴⁴ Kuna jambo moja ninalopaswa kuchunguza kabla sijaondoka, la sivyo sitajisikia kuridhika sana. Billy, Loyce, na wengineo sikuzote wananiambia, “Huji kwa wakati unaofaa.” Vema, si—sijui ni kwa nini.

⁴⁵ Kwa hiyo, usiku wa leo, Billy anasema sababu yake ni, kasema Dada Anna Jeanne alikuwa ametunga wimbo, aliandika wimbo kuhusu *Nakupenda Yesu*, ama kitu fulani. Sijui kama ningeweza kusikia pambio ndogo ya huo kabla sijahubiri. Je, mngeipenda hiyo, mwifurahie pamoja nami?

⁴⁶ Wimbo huo ni upi? [Ndugu fulani anasema, “*Asante, Yesu.*”—Mh.] *Asante, Yesu*, ndio huo. Huo ndio, *Asante, Yesu*. Ningependa kuusikia. Je, mngependa kuusikia pamoja nami? Nataka tu dakika chache... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Siamini... [Sehemu tupu kwenye kanda.]

⁴⁷ Sasa, nitaandika, nimwambie Ndugu Outlaw afadhali aufanyie mazoezi ule *Juu, Juu, Juu*. Endelea na huo, Dada Anna Jeanne, hilo ni sawa. Yeye ni msemaji, mkaguzi, nami sijui yote, na sasa yeye ni mshairi, mtunzi wa nyimbo. Hilo ni jema.

⁴⁸ Nami...Ndugu Moore alikuwa tu akiniambia jinsi alivyokuja, na, “Yeye alinileta mbali sana kutoka...?...” Huo ni mzuri sana. Mnajua inahitaji moyo kulilia jambo fulani upate kulifanya halisi. Mnaona? Jambo ndilo hilo, wakati moyo unapolia.

⁴⁹ Vema, ninawashukuru tu kwa ushirikiano wenu wote, kwa yote, kila kitu ambacho mmefanya. Mungu awabariki. Na mniombee sasa. Nasi tutawaombea wagonjwa katika dakika chache tu. Nami ni—nina lesa hapa, lakini, za kuombewa. Na

mama mmoja mweusi aliniambia ya kwamba alikuwa na lesu humu ndani ya mpendwa fulani, naye ameketi karibu na mama mmoja. Mnajua, mtu yeyote, akija, aangalie huko juu, huwezi kujua kama watu hao ni weusi au weupe kutoka hapa. Hiyo ni kweli. Lakini Roho Mtakatifu alikuwa na hao watu hapa nje wakitembea mbele yangu, na hiyo ndiyo sababu nilijua walikuwa weusi, watu weusi.

Mtu fulani akasema, “Sasa, ungewezaje kuwaona *huko juu*?”

⁵⁰ Nikasema, “Sikuwaona, nimewaona *hapa* nje.” Mnaona? Hiyo ni kweli. Ilikuwa ni *huku* nje. Nao walikuwa wameketi pale kwa imani wakiamini, ndipo Mungu akafanya kazi, hivyo tu. Hiyo tu ndiyo inavyohitajika, kuwa tu na imani, na uamini.

⁵¹ Na sasa, kama wakati wowote ninaweza kuombea lesu, ama chochote kwa ajili yenu, niandikieni tu huko Jeffersonville, nami nitafurahia kuwatumia moja kwa moja, bila malipo, bila gharama yoyote. Na hivi karibuni tuna vitabu vinavyokuja, nami, Ndugu Jack aliniambia, sipendi kutangaza mikutano yangu mwenyewe ma—mahali kama hapa, lakini sasa, kama una wapendwa walio karibu na Jeffersonville, juma lijalo, kuanzia Jumapili ijayo, kwenye Maskani mimi, Jumapili ijayo asubuhi, ninachukua mlango wa kwanza wa Ufunuo kutoa mandhari, kule kufunuliwa kwa Ufunuo.

⁵² Sasa, *ufunuo* katika neno la Kiyunani unamaanisha kama, “kuondoa ki—kitambaa kutoka kwenye sanamu, ku—kuifunua.” Mnaona? Na hiyo ni *Kufunuliwa Kwa Yesu Kristo Katika Nyakati Saba Za Kanisa*. Nami ninaandika maelezo madogo juu yake. Siwezi kuliandika, bila shaka, bali inanibidi tu kulinena chini ya uvuvio, ninapolipokea, halafu basi, bila shaka, watalinasa kwenye kanda ya sumaku, kisha kutoka hapo wayaandike kwa hatimkato, kwa hatimkato kisha wayapige chapa. Na sasa, tutakuwa na kanda, halafu pia tutakuwa—tutakuwa—tutakuwa nayo katika kitabu hivi karibuni, Bwana akipenda. Halafu labda wakati mwingine nitakapokuja huku tutakuwa navyo.

⁵³ Kwa hiyo, kama mko karibu na hapo, yeyote wa wapendwa wenu, waambieni waingie. Sasa, tu—tunajaribu kupata nafasi ya kutosha kuwashughulikia watu, maana ndio kwanza nitangaze papo hapo, lakini tayari tumesikia nasahau ni majimbo mangapi yako huku, mnaona, kwamba watu wanaingia, tayari wamehifadhi nafasi, wanakaa kwa juma hili namna hiyo.

⁵⁴ Jumatatu usiku itakuwa kwenye kanisa la Efeso, halafu Smirna, na Sardi, na kuendelea, Thiatira, na kuendelea hadi Jumapili asubuhi, juma zima, nitakuwa nikizungumza juu ya kanisa la Laodikia. Na hapo katikati, jinsi ambavyo kuna mlango uliofunguliwa uliowekwa kati ya Wakati wa Kanisa la Filadelfia na wa Laodikia, na huo ndio mlango

tunaotaka kuzungumzia, kwenye, kwenye ibada hiyo. Sasa Bwana awabariki, nanyi mwe mkiniombea.

55 Sasa kabla hatujalikaribia Neno kuu, Neno la Mungu, Neno lisilokosea... Imani yangu imejengwa kwa uchaji juu ya Neno hili. Wakati Neno hili linaposema jambo hilo, basi ni—ninaliamini tu, si—sijaribu kuongeza chochote kwake, wala kuondoa chochote kutoka kwake.

56 Na asubuhi ya leo huenda i—ikanibidi kuwaomba msamaha hawa, baadhi ya watu hawa wazuri hapa kuhusu baadhi ya matamshi hayo fidhuli kuhusu nyumbu kuwa haramu. Lakini sikukusudia kuwa fidhuli au kukufuru, bali nilikuwa tu nikijaribu kutoa hoja. Mnaelewa, sivyo?

57 Chochote, nyumbu, loo, jamani, hivyo ndivyo mwanadamu alivyofanya. Mnaona? Hawezi—hawezi kurudi, ha—ha—hawezi kwenda mbali zaidi. Yeye—yeye—yeye hajui baba yake ni nani, mama, yeye kabisa—yeye kabisa—yeye kabisa hana matumaini, hivyo tu, hakuna lingine. Ha—hawezi kujizaa tena, kwa hiyo yeye ananinii tu... Lakini mnajua, kwa kweli, yeye hana ninii... Yeye atangojea maishani mwake mwote apate kukupiga teke kabla tu hajafa, na kukuua, akiweza, hakika atafanya hivyo. Yeye—yeye atasubiri tu maishani mwake mwote, akikuvizia, akingojea tu, “Nitakupata huku nyuma yangu, siku moja.”

58 Na hivyo ndivyo tu watu wengi kanisani wako hivyo. Hiyo ni kweli. “Loo, nitakupigapiga mgongoni, mpaka nitakapopata nafasi ya kukata koo lako.” Mnaona?

59 Lakini mnajua, napenda farasi, sivyo? Loo, hasa farasi ukoo safi, mmoja ambaye—ambaye anawajua wahenga wa—wake, kwamba wao ni akina nani, walikotoka, kuanzia baba, mama, babu, babu wa babu, babu wa babu wa babu, huko nyuma kabisa, anajua mkondo wake wa damu. Unaweza kumwamini.

60 Hivyo ndivyo ilivyo kwa—kwa Mkristo. Ni... Ninapenda Mkristo ukoo safi, Mkristo aliyezaliwa na Roho Mtakatifu, si kutokana na kanuni fulani ya imani, bali anajua anatoka kwenye mkondo gani wa Damu. Yeye ni Mpentekoste wa kweli, ukoo safi, kote, amezaliwa na Roho Mtakatifu, kote huko nyuma hadi Pentekoste, ujuzi wake, napenda hilo, Mkristo ukoo safi. Anajua alikotoka, anajua Baba yake ni Nani, Mama yake ni Nani, Mwokozi wake ni Nani, na Mungu wake ni Nani. Amina. Mkristo halisi ukoo safi, napenda hilo. Na kwa hiyo, hiyo ndiyo tofauti.

61 Nyumbu, hajui, yeye huinua tu masikio yake, wala hawezi kujifunza chochote, hajui chochote, na, yeye ni kiumbe, sawa.

62 Sasa, mnalipenda Neno la Bwana? Loo, jamani! Ni ajabu.

63 Sasa, nitazungumza usiku wa leo juu ya uponyaji wa Kiungu, Bwana akipenda, kidogo kwenye mstari huo. Lakini hebu tufungue sasa, katika Mathayo mlango wa 12 kwa ajili ya fungu

dogo, na kisha kutoka kwenye hili tutoe muktadha, Bwana akipenda. Mathayo mlango wa 12, na sasa hebu tuanze kusoma kwenye kifungu cha 38 cha Mathayo mlango wa 12, kwenu mnaoliandika somo. Kama vile mara nyingi watu mikutanoni hufanya, wanaliandika somo, na—na kwa namna wanaliweka niani mwao, ndipo wanapopata hizo kanda wanazirudia-rudia, na kadhalika.

Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.

Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara; wala hakitapewa . . . ishara, ila ishara ya nabii Yona:

Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la . . . tumbo la nyangumi; ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

Malkia wa kusini atasimama . . . siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapozungumza na Mwandishi wake.

⁶⁴ Bwana mwenye rehema, Maneno haya yalinakiliwa na mwandishi, Mathayo. Ni Neno Lako Mwenyewe, nasi tunajua Neno Lako ni Uzima. Ni hukumu kwa asiyeamini, na Uzima kwake aaminiye.

⁶⁵ Tunaomba, Bwana, kama kuna wasioamini wowote, kwamba watakuwa waaminio usiku wa leo. Kama kuna yeyote mgonjwa, jalia waponywe. Kama kuna yeyote aliyechoka, jalia wafanywe wenye furaha; bila furaha, furaha zote zilitoka kwenye visima vyao, jalia upendo wa Mungu ukikandike kisima hicho tena, na mvua ya Mungu ikimwagikie. Tujalie, Bwana.

⁶⁶ Utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tuwasameheavyo waliotukosea. Nasi tungeomba, Bwana, ya kwamba ungetupokea kama watumishi Wako. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utatupa upeo mkubwa kwenye siku hizi chache za kongamano na mikutano hapa. Jinsi tunavyokushukuru kwa yale ambayo tayari yamefanywa!

⁶⁷ Na sasa, tunaomba ya kwamba hakutakuwako na mtu mmoja mnyonge atakayesalia miongoni mwetu, dhaifu kiroho, au dhaifu kimwili. Jalia nguvu zilizomfufua Yesu Kristo kutoka

kaburini, ziingie katika kila moyo usiku wa leo, wape ukombozi kutoka kwa dhambi na kutokuamini, wape ukombozi kutoka kwa magonjwa na mateso. Na jalia tuweke kando kila kitu kidogo, tutazame moja kwa moja Kalvari sasa, na kupokea baraka za Mungu.

⁶⁸ Ninaamini ya kwamba mkutano huu ulikusudiwa na Wewe. Nami ninaamini ya kwamba mambo yataibuka kwenye mkutano huu ambayo hatuyafahamu bado, lakini katika siku zijazo, kwamba tutaona ya kwamba mkutano huu uliletwa na hekima ya namna nyingi ya Mungu. Wamishenari watakuwa wakiondoka hapa, kuwa pamoja nao, Bwana. Miito imetolewa kwa watu, ishara kuu na maaajabu ya Bwana aliyefufuka zimefanywa, roho zilizokuwa juu ya watu katika siku zilizopita ambao umewatumia zimejidhihirisha miongoni mwetu, hasa sana Roho Mtakatifu.

⁶⁹ Baba, tunaomba ya kwamba utambariki Ndugu Moore, Dada Moore, na wote wanaohusika na maskani hii, waongoze na kuwaelekeza. Kila mhudumu, mmishenari, ama yeyote yule katika jengo hili usiku wa leo, ama aliyekuwa hapa ndani, jalia wawe wamepokea kitu kitakachowavuvia kusonga mbele upesi, kwa kuwa ile saa inakaribia.

⁷⁰ Ndipo wakati utakuja ambapo hakutakuwa na kazi nyingine tunayoweza kufanya, hivi karibuni itakatiliwa mbali kutoka kwetu, tunapooni tunda likififia, Mzabibu ukisafishwa. Ninaomba, Baba, ya kwamba utatujalia baraka hizi kupitia Yesu Kristo Bwana wetu, tunaomba, katika Jina Lake. Amina.

⁷¹ Ninataka kutumia maneno matano kwa ajili ya somo: *Malkia Wa Kusini*. [English: *The Queen Of The South—Mfa.*]

⁷² Huenda mtu fulani akasema, “Vema, hilo si ni somo dogo kwa ibada yako ya kumalizia?”

⁷³ Naam, kwa namna fulani ni fungu dogo, hiyo ni kweli, bali linatoka kwa Biblia ndiyo inayolifanya zuri. Mnaona, si ukubwa wake, ni ubora wake; sio wingi, ni ubora.

⁷⁴ Kama nilivyosema mara nyingi, maskini rafiki mmoja wakati mmoja, akitafuta kwenye dari, aliingia kwenye kasha la kale, naye akapata stempu ndogo ya posta ambayo, basi akawazia angepata nikeli moja kutoka kwake akajinunulie aiskrimu. Naye alikuwa akiipeleka kwa mkusanyaji wa stempu, naye akampa dola moja, hilo lilimridhisha huyo mvulana mdogo. Na kwa hiyo, huyo mkusanyaji wa stempu akaiuza kwa mamia ya dola, na sasa nafikiri imefikia mamia, mara mamia ya dola, maskini stempu ndogo, ya manjano. Sasa, kuhusu hiyo karatasi, haikuwa na thamani yoyote, bali ni kile kilichokuwa kwenye hiyo karatasi kilichojalisha.

⁷⁵ Sasa, *Malkia Wa Kusini* ni maneno matano tu, wala si hiyo karatasi yaliyoandikiwa, ni thamani ya hilo Neno lililoandikwa kwenye hiyo karatasi. Biblia nzima nilipewa na Ndugu Kidson

miaka mingi iliyopita, nayo Biblia labda ingegharimu kama dola ishirini na tano, Biblia ya Scofield. Lakini ni, *Hili* hapa litaondoa ama Uzima au mauti kwetu; na katika Hilo mna msamaha kwa kila mtu atakayelisikia, na ni hukumu kwa wale wasiolisikia.

⁷⁶ Wakati mmoja Abraham Lincoln mashuhuri aliitwa kuchukua hatua. Mtu mmoja alihukumiwa adhabu ya kifo chini ya kikosi cha kupiga risasi kwa hatia ya kutoroka jeshini, ama kitu fulani, alikuwa na kile walichokiita, “kutorokea kilimani,” ama kufanya kosa fulani la kijeshi, naye akahukumiwa kufa. Basi mtu huyo alishikwa tu na wasiwasi na hofu, naye akahukumiwa, hata hivyo, na baadhi ya majemadari katili, ama kitu fulani, kwamba alikuwa afe.

⁷⁷ Rafiki yake mwema akakimbia kwa Bw. Lincoln, basi alipokuwa akitoka kwenye gari lake kuingia chumbani mwake, akamwambia, “Mtu huyu ni mtu mzuri, yeye hata ni Mkristo. Na yeye—yeye, Bw. Lincoln, wewe ni Mkristo, naye atakufa! Atakufa kesho asubuhi mbele ya kikosi cha wapiga risasi. Bwana, wewe ukiwa ni Mkristo, na unajua hali ya mtu huyu, hakukusudia kukiuka sheria zozote, aliogopa alipofika vitani. Wewe ndiwe tu unayeweza kumwoko.”

Bw. Lincoln alinyakua tu kipande cha karatasi, akaandika pale, “Amesamehewa. Abraham Lincoln,” akakirudisha.

⁷⁸ Na kwa hiyo alipofika kwenye seli za gereza ambako rafiki yake alikuwa akingojea, alisema, “Loo, Mungu ashukuriwe, umesamehewa! Bw. Lincoln alikusamehe.”

⁷⁹ Kwa hiyo, anaangalia kote, anaangalia hiyo karatasi, akasema, “Kwa nini unifanyie mzaha sasa, wakati ninakaribia kufa chini ya kikosi cha kupiga risasi?” Kasema, “Huyo si Abraham Lincoln.” Kasema, “Hiyo si sahihi ya—yake. Kama ningepata msamaha kutoka kwa Abraham Lincoln,” kasema, “ingekuwa, mbona, ingeandikwa, na kutiwa muhuri, na kila kitu.” Akasema, “La, huo hauko kwenye karatasi ifaayo.” Kasema, “Si—sitaupokea huo.”

⁸⁰ Kesho yake asubuhi mtu huyo akafa, kwa kuwa alikuwa amehukumiwa kufa. Sasa, hapa mtu huyu ameshika msamaha wa Abraham Lincoln asipigwe risasi, halafu akapigwa risasi. Ilisikilizwa katika mahakama za shirikisho, na huu hapa uamuzi wao: “Msamaha si msamaha, isipokuwa upokewe kama msamaha.”

⁸¹ Hilo ni Neno la Mungu, ni uponyaji kwa wale wanaoweza kuupokea kama uponyaji, bali si uponyaji kwa wale wasioweza kuupokea kama uponyaji; ni msamaha wa dhambi kwa wale wanaoamini ya kwamba wamesamehewa dhambi, bali halina faida kwa wale ambao hawatalipokea namna hiyo.

⁸² Ahadi ya Roho Mtakatifu ni hakikisho kwako ya kwamba utampata kama ukimpokea hivyo, inategemea mtazamo wako kwa Neno. Neno ni, sio karatasi, ni kitabu tu, bali ni—ni Kristo

aliyedhihirishwa kwenye karatasi. Hivyo ndivyo ilivyo. Mungu, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Mnaona? Nayo Maneno Yake ni Roho na Uzima.

⁸³ Tunalipokea tu Neno Lake kama tu kwamba ilikuwa ni Yeye Mwenyewe. Ninapoiona ahadi Yake, kwangu mimi hiyo ni Kristo, ninaikumbatia. Yeye hawezi kusema uongo. Kwa—kwangu mimi hiyo ni kweli kabisa. Mnaona? Huenda nisijue jinsi ya kulishika, bali ni kweli, nami ninalishikilia moja kwa moja kwa sababu ni Kristo kwangu.

⁸⁴ Katika somo letu, usiku wa leo, tunamwona Yesu akilikaripia na kulikemea kundi la watu waliokuwa wamekataa kuamini kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, ingawa alikuwa amefanya ishara nyingi za Masihi miongoni mwa watu. Nao walikuwa wamemwita vifungu viwili tu vilivyotangulia nyuma ya hiki, Beelzebuli, Naye akasema, “Mkiniita jina baya, nitawasamehe. Mnaponiona nikifanya...” Hebu kwa namna fulani nifasiri hivi, kusudi mpate ninalomaanisha, “Mnaniita Mimi, ninapowaonyesha kazi za Mungu, mnaniita Beelzebuli.” Sasa, *Beelzebuli* ni kama mpiga ramli, ibilisi. “Mnaniita Beelzebuli, nitawasamehe hilo,” mnaona, “lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja kufanya jambo lile lile, nanyi mkinena dhidi ya Huyu, kamwe halitasamehewa katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.”

⁸⁵ Huo ndio uzito wa yale tunayopitia siku hizi. Mnaona? Loo, Yeye, Naye aliwakemea kwa sababu hawakuwa wamempokea, na akisha kufanya kazi za Mungu, na kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.

⁸⁶ Sasa, kama Yeye alinena Maneno hayo, Hayo ni kweli kabisa. Ndipo katika siku hii tunayoishi, ambapo Roho Mtakatifu amekuja, na kufanya kazi zile zile tena, mnaona mahali tunaposimama usiku wa leo? Ni—ni jambo la kuchukiza sana kuwazia ya kwamba watu siku hizi wangali wataiita kazi ya Mungu ibilisi. Naye Yesu alikuwa akiwakemea.

⁸⁷ Sasa, kama tutarudi nyuma kidogo katika Biblia, tutaona ya kwamba Mungu katika nyakati zote, wakati wote amekuwa na karama katika Kanisa Lake. Hapajakuwapo na wakati pasipo Mungu, anapoingia Kanisani Mwake, mambo ya kimbinguni hufanyika.

⁸⁸ Ninajua ninazungumza na wanahistoria, Ndugu Moore ni mmoja wao, hodari kama niliopata kujua, yeye mwenyewe. Na wakati wowote ambapo Kanisa liliwahi kuwa na uamsho, daima ishara ya kimbinguni imo humo mkutanoni: Mungu huwaponya wagonjwa, hunena kwa lugha, na kufanya miujiza mingine na ishara, kila wakati waliowahi kuwa na uamsho. Na hata kabla ya kuja kwa Kristo, kila wakati Mungu alipotuma kitu cha kimbi-..., ama, huduma miongoni mwa watu, ishara za

kimbinguni zilikuwa miongoni mwao. Kwa hiyo, mnaona, sisi ni wa kiinjalisti, tunaamini, tunaamini kabisa ya kwamba Mungu anaishi katika Kanisa Lake na katika watu Wake, tunaamini hilo. Naye anaonyesha ishara ya furaha, na nguvu za Mfalme kambini.

⁸⁹ Kwa hiyo, katika nyakati zote walikuwa na ishara za kila namna, Naye akarejelea baadhi yake hapa. Mojawapo Yeye akasema, “Kama ilivyokuwa katika wakati wa Yona,” akamwita Yona. Sasa, watu wengi wanamhukumu maskini Yona, naye Yona alikuwa ni nabii, lakini sikuzote nilimhurumia, kwa sababu wengi sana siku hizi wanamhukumu Yona na kusema alikuwa nje ya mapenzi ya Bwana. Kwa hiyo nitamtetea Yona na kusema hakuwa nje ya mapenzi ya Bwana. Mimi... Ninyi angalieni mwone sasa, tutaenda kuyachukua maisha yake kwa dakika chache, na kuyachunguza.

⁹⁰ Yona alikuwa akienda—akienda zake Ninawi, bila shaka. Nayo Biblia inasema ya kwamba hatua za mwenye haki zinaongozwa na Bwana, basi Yona asingeweza kufanya lolote, akiwa nabii, bila Mungu kumwongoza.

⁹¹ Nimefanya mambo mimi mwenyewe, nanyi pia, mlidhani ilikuwa ni upumbavu, kweli, yale mliyowazia yalikuwa sahihi, lakini mkaja kugundua ilikuwa ni kweli kabisa. Mnaona, Mungu daima hufanya hivyo kwa sababu Yeye huwaongoza wenye haki. Uaenda tu jinsi Roho aongozavyo.

⁹² Naye Yona akapata shida huko baharini, nasi tunajua jinsi hiyo hadithi inavyosema, kwamba alikuwa amefungwa mikono na mguu, na kutupwa nje ya meli, ndipo samaki akaja, akamchukua, kama tunavyomwita nyangumi. Naye akashuka chini ya kilindi cha bahari baada ya kumla Yona, kummeza. Naye akashuka chini ya bahari, na kwa hiyo wao...

⁹³ Hiyo ni hadithi ambayo daima huishangaza sayansi, maana sayansi inasema kwamba koo la nyangumi si kubwa vya kutosha kumeza mtu, lakini ukiangalia Biblia ilisema ya kwamba Mungu alimweka huyu tayari, huyu alikuwa ni sa—sa—samaki maalum. Mungu, Yeye ni Yehova-Yire, Yeye anaweza kutoa chochote anachotaka kufanya, kwa sababu Yeye ni Mungu. Ibrahimu alimwita Yehova-Yire, maana Yeye alinena dhabihu hiyo ikawa. Yeye angali ni Yehova-Yire, Yeye anaweza kutoa anachotaka. Naye alimwandaa samaki huyu.

⁹⁴ Msichana mdogo, mwenye furaha, wakati mmoja akitoka kanisani pamoja na Biblia yake, alikuwa anaenda zake, kafiri akakutana naye, na kusema, “Kwani unafurahia nini hivi?”

Kasema, “Ndio kwanza niokoke, Yesu yuko moyoni mwangu.”

Kasema, “Upuuzi.” Kasema, “Umeshika nini hapo, Biblia?”

Kasema, “Ndiyo.”

Kasema, “Nadhani unaamini ile hadithi ya nyangumi na Yona.”

Kasema, “Loo, naam, ninaiamini, kila Neno. Yale Mungu asemayo ni kweli.”

Akasema, “Vema, utathibitishaje jambo hilo, vinginevyo ila kwa imani?”

Akasema, “Nitakapofika Mbinguni, nitamwuliza Yona.” Uh-huh. Hiyo ni kweli.

Akasema, “Basi, vipi kama Yona hayuko huko?”

⁹⁵ Kasema, “Basi umwulize wewe.” Hilo ni wazo zuri basi. “Mwulize wewe.” Vema. Mungu daima analo jibu, kama tu utafungua kinywa chako Yeye anapokifungua.

⁹⁶ Mungu alimwandalia Yona samaki maalum, naye akammeza, ninaamini hilo, kila Neno lake. Naye akashuka baharini, basi samaki anapokula, hebu mlishe maskini samaki wako wa dhahabu, utamwona, anashuka moja kwa moja chini, aweke maskini pezi zake chini ya hilo bakuli la samaki. Uliwahi kumlisha? Akijaza maskini tumbo lake, hushuka moja kwa moja, anapumzika chini ya bakuli la samaki. Samaki hufanya hivyo, baada ya kutoka na kwenda kula, anarudi moja kwa moja juu ya kiota na kupumzika.

⁹⁷ Vema, nyangumi huyu alikuwa amemmeza nabii huyu, akashuka chini ya bahari kupumzika. Naye huyu hapa Yona alikuwa akigaagaa kote katika matapiko hayo, huko chini ya bahari. Na sikuzote nilifikiri. . .

⁹⁸ Watu husema, “Mbona, mkono wangu haujapata nafuu, wala m—mguu wangu si bora. Sijisikii afadhali hata kidogo.”

⁹⁹ Kamwe hutajisikia afadhali hata kidogo ukiangalia hizo, unaangalia dalili zako. Maadamu unaangalia dalili zako, hutaona kitu kingine chochote ila dalili zako. Inategemea kile unachoangalia.

¹⁰⁰ Sasa mwangalie Yona, sasa, alikuwa katika hali mbaya sana; hakuna mtu hapa katika maskani hii aliye na hali mbaya hivyo usiku wa leo. Alikuwa katika tumbo la nyangumi, kama aliangalia upande *huru* ulikuwa ni tumbo la nyangumi, kila mahali alipoangalia palikuwa ni tumbo la nyangumi, naye akasema, “Ni ubatili wa uongo. Mara nyingine tena nitalitazama hekalu Lako takatifu.”

¹⁰¹ Kwa kuwa alijua ya kwamba wakati Sulemani alipoliweka wakfu hekalu lile, mbona, aliomba na kusema, “Bwana, kama watu Wako wakipata shida mahali popote, na kulikabili hekalu hili takatifu, na kuomba, basi Wewe sikia kutoka Mbinguni.” Naye aliamini maombi ya Sulemani yangejibiwa. Kwa hiyo, Mungu akamfanya huyo samaki mgonjwa ageuke moja kwa moja, na kumpeleka Yona kwenye nchi kavu.

¹⁰² Sasa, kama Yona, chini ya hali hizo angeweza kuangalia hekalu ambalo lilijengwa na mwanadamu, Sulemani, ambaye baadaye alirudi nyuma, hekalu la duniani, na maombi ya mtu wa kawaida, naye Mungu angeweza kumfanyia mwujiza kama huo, ni zaidi sana jinsi gani anavyoweza kutufanyia mimi na wewe tunapokataa kuangalia hali zetu! Basi mara nyingine tena nitaangalia kwenye Hekalu Takatifu ambapo Yesu ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu akituombea tunapokiri. Amina.

¹⁰³ Tunaweza je kuangalia dalili? Ninamwangalia Yesu. Si jinsi—sio jinsi *hii* inavyoonekana, bali vile *Hilo* lilivyosema. Angalia Kalvari, angalia gharama iliyolipiwa.

¹⁰⁴ Mtu alikuja akasema, “Mimi ni duni sana, Ndugu Branham, Mungu kamwe hawezi kuniokoa.”

¹⁰⁵ Usiangalie jinsi ulivyo mbaya, angalia jinsi Yeye alivyo mwema. Kamwe usijiangalie, mwangalie Yeye. Kuhani kamwe hakuona yu—yu—yule aliyetolewa dhabihu.

¹⁰⁶ Kama vile Ndugu Bosworth alivyozea kusema juu ya maskini nyumbu wake, kasema, “Nyumbu angezaliwa, nayo masikio yake yalikuwa yameinama, mkia wake umetokeza, na magoti yake yana matege, nayo macho yake yana makegeza.” Kasema, “Vema, kama angeweza kuzungunza angesema, ‘Vema watakapotoka, watanigonga kichwani, kwa sababu, hawatanilisha, mimi sistahili kulishwa.’

¹⁰⁷ “Lakini kama mama yake alikuwa amefunzwa vizuri, angesema, ‘Mwanangu, huna haja ya kuwa na wasiwasi, ulizaliwa chini ya haki ya mzaliwa wa kwanza. Itabidi kuwe na mwana-kondoo asiye na ila atakayekufa kwa ajili yako, upate kuishi.’”

¹⁰⁸ Na hiyo ni kweli kabisa. Kuhani kamwe hakumwona huyo nyumbu, hakumchunguza huyo nyumbu, alimchunguza huyo mwana-kondoo. Si ila juu ya huyo nyumbu, ila, kama kulikuwa na ila yoyote juu ya huyo mwana-kondoo. Kwa hiyo kama huwezi kupata ila yoyote juu Yake, unahofia nini basi? Si wewe, ni Yeye. Mungu hakuangalii wewe, anamwangalia Yeye. Mnaliona? Unaliona, dada? Unaliona, ndugu, uliyeketi hapa? Unaliona? Hakuangalii wewe, Yeye anamwangalia Kristo, hiyo ndiyo Dhabihu, Yeye huiangalia ile Dhabihu.

¹⁰⁹ Kwa hiyo Yona, kuendelea pamoja naye, tunaona ya kwamba watu wa Ninawi walikuwa waovu sana. Ninaambiwa walikuwa waabudu sanamu, nao waliabudu wanyama, naye mungu wa bahari alikuwa nyangumi, na kazi yao ilikuwa ni kuvua samaki. Kwa hiyo, wakati watu wote walipoenda kazini asubuhi hiyo, jiji lenye ukubwa wa karibu St. Louis, walipoenda baharini na mitumbwi yao, huyu hapa mungu wa baharini akaja akiviringika kuingia ukingoni, akatoa ulimi wake kama ubao

wa kutokea, huyu hapa nabii akaja, akitoka moja kwa moja kinywani mwake.

¹¹⁰ Si ajabu walitubu. Mnaona? Naam. Hakika. Walitubu kwa sababu mungu wao alikuwa amewapelekea nabii kwa ishara ya kimbinguni. Amina. Si ajabu Yeye alisema atakihukumu kizazi hiki, hao watu katika wakati wa Yona.

¹¹¹ Ninataka kuingiza hili kidogo, pia, tunapoendelea, kama litawasaidia, angalieni, Yeye alisema, “Na watu wa Ninawi watasimama katika kizazi hiki, na kukihukumu kuwa kimekosa, kwa sababu walitubu kwa mahubiri ya Yona, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.”

Sasa angalieni, walipokwisha kumwuliza, Yeye alisema, “Kutakuwako. . .”

¹¹² Kasema, “Tupe ishara,” baada ya mambo mengi sana aliyokuwa amefanya. Mnamwona huyo ibilisi? Kama tu alivyosema, “Fanya mwujiza hapa, na uyageuze mawe haya yawe mkate.” Wakamfunga kitambaa usoni Mwake, wakampiga kichwani, kasema, “Tuambie ni nani aliyekupiga, tutaamini. Wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga.”

¹¹³ Ibilisi yuyo huyo atafanya vivyo hivyo, “Mponye huyu *hapa*, hebu nikuone ukimponya.” Mnaona hapo, huyo ni ibilisi yuyo huyo anayeishi ndani ya watu wa kidini. “Hebu nikuone ukifanya mwujiza. Sitaninii. . . Mzee *Nanii* anauza penseli hapa chini pembeni, amekuwa kiwete. Hebu niwaone ninyi waponyaji wa Kiungu mkiponya.” Kumbukeni tu huyo ni ibilisi. Unaona?

¹¹⁴ Hatuwafanyii vitimbi, Mungu kamwe, Yona kamwe, hakuna mwingine anayefanya hivyo. Wao wananinii tu, “Waacheni, wao ni vipofu wakiongoza vipofu,” kwa hiyo usiwaambie chochote, endelea tu kusonga mbele. Tuna wengi zaidi wanaoliamini, kuliko kujipumbaza na wasioamini.

¹¹⁵ Lakini angalieni, Yesu alisema, “Kizazi kibaya na cha zinaa kitatafuta ishara; wala hawatapokea ishara yoyote, ila ishara ya Yona. Kwa maana kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku.”

¹¹⁶ Angalieni, sasa lipateni: Ni kizazi cha aina gani? Kiza- . . . kibaya, kiovu, cha zinaa. Alikuwa akinena juu ya kizazi *hiki*, ama kizazi chochote ambacho kingesema, “Nifanyie ishara, nionyeshe. . .” Hivyo ndivyo walivyokuwa wakimwambia.

¹¹⁷ Sasa, hawa jamaa siku hizi ambao hawaamini katika uponyaji wa Kiungu, na hawaamini katika miujiza wanauliza, “Hebu nikuone ukimponya *huyu*, hebu nikuone ukimponya *yule*,” Biblia ilisema wangepata ishara. Ingekuwa ni ishara ya namna gani? Ishara ya ufufuo. Haleluya! Tunayo, amina, iko hapa sasa.

¹¹⁸ Yesu Kristo amefufuka katika wafu, na yu hai baada ya miaka elfu mbili, akijionyesha Mwenyewe miongoni mwetu. Kizazi kibaya, cha zinaa, kiovu, kizazi cha zinaa ambacho ni kizazi *hiki*, kama Sodoma, tumekirudia tena. Yeye alisema, “Kizazi hicho kitatafuta ishara, nao watapata ishara, hiyo ishara itakuwa ni ya ufufuo.” Mnalipata?

¹¹⁹ Na sasa ndipo wanaiita, kuwafanya, kuwapeleka mbali zaidi na Mungu wanasema, “Ni ibilisi. Ni kusoma mawazo. Ni telepathia, ama kitu fulani,” bila kujua ya kwamba ni ufufuo kwa Yesu Kristo miongoni mwa watu Wake. Utukufu! Loo, kama ilivyokuwa katika siku za Yona! Mnaona? Wengi. . .

¹²⁰ Sasa tunakuja kwa Sulemani. Katika siku za Sulemani, msomaji yeyote wa Biblia anajua ya kwamba huo ulikuwa ni wakati wa upeo wa ufanisi wa Israeli. Hizo zilikuwa ndizo siku zao bora sana walizopata kuwa nazo, hizo zilikuwa ni Utawala wao mdogo wa miaka elfu moja, kila kitu kilifanikiwa chini ya Sulemani. Kwa nini? Mungu anapowapa watu karama, ama taifa, ama watu, nao watu hao wataitambua karama hiyo, ni wakati wa upeo wa ufanisi kwao. Wakiikataa, ni machafuko kwao. Hiyo ndiyo sababu Yeye aliendelea kusema, “Hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.” Nao walikuwa wakimkataa.

¹²¹ Vema, hebu tumchukue Sulemani kwa dakika chache. Sulemani alipewa karama ya upambanuzi, nao Israeli wote wakaiunga mkono, kila mtu aliiamini. Mbona, alikuwa na karama ya upambanuzi, naye angeweza kuwapambanulia watu. Na kila mtu alikuwa na moyo mmoja, na nia moja, kuizunguka hiyo karama kuu ya Mungu, “Mungu asifiwe, Yehova mkuu.” Waliimba nyimbo, wakajenga hekalu, wakafanya mambo makuu, maana walikuwa na furaha. Yehova alikuwa ameweka karama ya upambanuzi ndani ya mtu mmoja, Sulemani, nao wote waliifurahia.

¹²² Loo, laiti Marekani, usiku wa leo, ingeionga mkono karama ya Mungu, ingekuwa ni wakati wa upeo wa ufanisi, ingekuwa ni utawala wa miaka elfu kwa ajili yetu hapa. Vipi kama tungeionga mkono Karama ya Mungu? Yule, huyo ni Roho Mtakatifu, bila shaka. Marekani yote ingeionga mkono karama ambayo Mungu alitutumia, Roho Mtakatifu, ingekuwa ni wakati ambapo wangevunja kila ukuta wa farakano kati ya Wamethodisti, Baptisti, Presbiteri, Lutheri, Wapentekoste, nasi tungekuwa na wakati wa upeo wa ufanisi, na nguvu za Mungu zingefagia taifa hili kutoka bahari hadi bahari inayong’aa, kila taifa chini ya Mbingu lingetuogopa.

¹²³ Huo ndio ulinzi ulio bora kuliko wote tulio nao, ulinzi wa Mungu. Haitubidi kujenga mabomu ya atomiki, kushindana na Urusi katika mashindano ya makombora, ni kumrudia tu Mungu, kukubali Karama aliyotupa Yeye, bali hawatafanya hivyo. Mbona, hata huwezi kuwafanya wengi wa ndugu wa

Kipentekoste kufanya hivyo, sembuse Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki, Lutheri, na kadhalika. Huwezi kuwafanya wengi waiamini, hawaiungi mkono. Ni kitu gani kilichosalia basi? Machafuko. Mungu anaituma, ni juu yako kuipokea.

¹²⁴ Sasa, wakati ninii, karama hiyo ilipopokelewa, watu wote kwa moyo mmoja, mbona, kila mtu aliyepitia kule, wangewaambia, “Loo, kabla hamjaondoka, hamna budi kupanda juu. Mmesikia habari za Mungu wetu, Mungu wetu ni Yehova, Yehova Mkuu, aliyeziumba Mbingu na nchi. Loo, kabla hamjaondoka nchini mwetu, hamna budi kukaa muda mrefu vya kutosha kuona mmoja wa hiyo mikutano. Loo, m—mngeshangaa kuona jinsi nguvu kuu za Mungu zinavyokuja juu ya mtu, mwangalie jinsi anavyopambanua mambo kati ya mema na mabaya kwa watu. Mbona, mnapaswa kuona, ni ya ajabu sana!”

¹²⁵ Vema, watu wangukuja na kuliona. Na loo, mbona, mioyo yao ilikuwa imechangamka kabisa, na kuondoka. Pasipo na mtu anayezungumza, akisema, “Aa! Siamini hilo. Uh-um. Hiyo si ya Mungu.” Kila mtu alikuwa na moyo mmoja kwake.

¹²⁶ Kama watu wanaoitwa kwa Jina la Yesu Kristo, kama watu wanaoitwa kanisa la Kikristo, hao watu tu peke yao, wangukusanyika pamoja, na kuomba, na kukubali Karama ambayo Mungu ametutumia, kusingekuwako na neno moja baya kuhusu Kitu hicho. Mbona, kungekuwako na kumwagwa kwa ajabu sana kwa Roho Mtakatifu, mataifa yangesikia, vichwa vya habari, matangazo ya televisheni, yangeenea kote ulimwenguni, kama tungeweza tu kuipata, bali hawatafanya hivyo. Basi ni kitu gani kilichosalia? Bomu la atomiki linatungojea, hivyo tu, kwa asiyeamini, Yesu anatungojea *sisi*. Bwana ashukuriwe! Kuna njia ya kuepukia, “Wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina Lake.”

¹²⁷ Sasa, Sulemani, tunaona basi ya kwamba watu walikuwa wakizungumza, na, kila mahali. Halafu habari, hawakuwa na televisheni wakati huo, na magazeti, ninii, ilikuwa ni kutoka mdomoni hadi sikioni. Na kila wakati watu wangeenda katika taifa lingine, wangeleta habari, “Ee, Mungu, Yehova Mungu mkuu wa—wa Wayahudi! Mbona, hao watu wana nia moja. Nao walijenga hekalu kubwa, hujawahi kuona fahari kama hiyo, hujapata kuona umoja kama huo, hujawahi kuona nguvu kama hizo. Naye Mungu amemzuru mtu mmoja kule, nao wamemfanya Mfalme wao.” Hata hatuwezi kumfanya mtu kama huyo mchungaji. Kasema, “Tunamfanya Mfalme. Na, loo, ni nguvu kuu jinsi gani ambazo Mungu anatumia! Jamaa huyo, Sulemani, huko juu, Mungu anafanya jambo kuu.”

¹²⁸ Sasa, habari ziliendelea kuenea, mpaka siku moja zikafika huko chini kabisa Sheba. Sasa, huko ni mbali sana huko chini. Nayo misafara ingepita, mwajua, na—nao wangeninii,

wanapokuja kila msafiri akipita, bila shaka angekuja kuwaona wakuu wa mataifa. Nalo taifa hili dogo lilikuwa likitawaliwa na Malkia, aliyetitwa Malkia wa Sheba, anayetajwa hapa kama Malkia wa Kusini kwa sababu ilikuwa kusini mwa Palestina. Malkia wa Kusini, ilisemekana alikuja kutoka pande za mwisho za dunia. Hizo zilikuwa sehemu za mwisho kabisa za dunia *iliyojulikana*, katika siku hiyo. Alikuwa huko mbali kupita Jangwa la Sahara. Hebu ipimeni kwenye ramani zenu, mbali sana huko chini.

¹²⁹ Kwa hiyo, hatimaye habari zikamfikia. Na kila mtu aliyekuja kutoka Palestina angesema, “Aisee, ndio kwanza upitie Palestina, laiti ungaliona umoja wa watu hao. Mungu wao amemtia mtu mafuta, naye mtu huyo anafanya ishara za Mungu aliye hai, ishara ambazo mwanadamu asingeweza kuzifanya. Mungu wao hana budi kuwa ni Mungu halisi.”

Mwajua, imani chanzo chake ni... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹³⁰ “Lakini unapaswa kuona huyo Roho mkuu juu yake. Sijawahi kuona upambanuzi kama huo. Loo, haukosei, kila wakati ni ukweli hasa, unapaswa kuuona. Sijawahi kuona chochote kama hicho.”

¹³¹ Akaanza kuona njaa, akaanza kuona kiu. Loo, ninapenda hilo, kuona kiu. Loo, wakati unapoona kiu, kuna jambo fulani kukihusu! Huwezi kuzungumza na mtu kuhusu maji, mpaka aone kiu, lakini anapoona kiu, atakunywa kutoka mahali fulani, ana kiu.

¹³² Hapa wakati fulani uliopita nilikuwa nikisoma katika Zaburi 63, Daudi alisema, “Kwa kuwa fadhili zako ni bora kwangu kuliko uhai, nitalisifu Jina Lako.”

Nikawaza, “Daudi alimaanisha nini? *Uhai*, hicho ndicho kitu kikuu kuliko vyote kilichopo, kwa hiyo lazima kuwe na tafsiri mbalimbali za *uhai*.”

¹³³ Sasa, watu wengine wanafikiri *maisha* ni kunywa pombe, na sherehe, na kuranda-randa, lakini maisha ya namna hiyo yana huzuni. Hatimaye... Hakuna... Hayo siyo aina ya maisha ambayo Daudi alikuwa akizungumzia. Sasa, wakati mwingine maisha ya namna hiyo yatakufanya uchukue bastola, na kulipua ubongo wako, uruke kutoka kwenye daraja na kujiua. Watu wanafikiri kwa sababu, “Jamani, kama ningeweza tu kupata dola milioni moja, hayo kweli yangekuwa ni maisha.” La, hayo ni mauti.

¹³⁴ Hapa wakati fulani uliopita nilikuwa pamoja na Ndugu Sothmann katika kanisa moja kuu, uwanja wa michezo huko Canada, kwenye jiji fulani kubwa. Nao ulikuwa ukiendelea vizuri sana, mpaka Wamarekani wakaja, nao wakaja kule, chama fulani. Ndipo usiku huo nilipoingia kwenye lifti, nikirudi

nyumbani kutoka mkutanoni, kulikuwa na chupa za wiski za kutosha mle kujaza sanduku moja au mawili ya wiski.

Nami nikamwambia yule mvulana mdogo aliyekuwa akinipandisha juu, nikasema, “Ni kitu gani hicho?”

¹³⁵ Akasema, “Wametoka ng’ambo ya mpaka, hapa juu.” Kasema, “Shirika fulani lina, chama fulani kina, kinafanyia yubile yao hapa.” Kasema, “Imekuwa ya kuchukiza sana.” Kasema, “Wewe ni Ndugu Branham?”

Nikasema, “Naam.” Nikasema, “Kwa namna fulani inanifanya nione aibu kuwa Mmarekani.”

Akasema, “Vema, wanayo hapa, pia.”

¹³⁶ Kwa hiyo, nikapanda juu na nikatoka kwenye lifti, basi nilipotoka kwenye lifti, nikasikia kitu fulani upande wa pili wa chumba, ukumbi mrefu, hoteli hii kubwa. Nikaangalia kule juu, na hawa hapa wanawake wawili wakishuka kupitia pale, yapata tu umri wa miaka ishirini na mitano, thelathini, wamevaa tu nguo zao za ndani, huku wanaume wakiwavuta, namna *hiyo*. Walikuwa na chupa ya wiski mkononi mwao, na wote wawili wamevaa pete za arusi; mume wao akiwalea watoto, labda, nyumbani. Loo, walikuwa tu na “maskini burudani safi.” Si ajabu tumeangamia. Labda walikuwa ni wa shule ya Jumapili, mahali fulani, ama mwalimu wa shule ya Jumapili.

¹³⁷ Ndipo wakashuka, nao jamaa hawa wamelewa sana, wakitambaa kwa magoti yao huku wakijaribu kuwashika, na kuvuta nguo chache walizokuwa wamevaa, wazivue. Nao wakashuka kule, nao wakawaondokea, wao... Nami nikarudi kwenye ule ukumbi mdogo kwenye kivuli. Ndipo mmoja wao akachukua wiski hii, na kunywa funda kubwa mno, namna *hiyo*, kisha akampa huyo mwingine, akavuta maskini sketi yake ya ndani, na kusema, “Whoopee! Haya ndiyo maisha!”

Nikasimama pale kidogo, nikatoka nje, nikasema, “Samahani! Hayo ni mauti!”

Akasema, “Karibu pombe.”

¹³⁸ Nikawashika kwa mkono, nikasema, “Angalieni hapa hizi pete za arusi. Hivi hamjionei aibu? Hata kama mngekuwa si chochote ila raia wa Marekani, ni fedheha kwa nchi yetu, na bendera yetu, na kile babu zetu walivyolianzisha taifa hili lipate kuwa! Mimi ni Mmarekani, pia, mimi ni mhubiri wa Injili.”

Wakaanza kuruka, na kuvuta, na kuruka, wakikoroma, kunirushia mateke, na chochote kile, kisha wakaondoka, wakashuka ukumbini.

¹³⁹ Hayo si maisha, hayo ni mauti! Ni kitu gani kinachofanya ninii, msichana mrembo angataka kufanya jambo kama hilo kwa sababu gani? Ni kwa nini mwanamume, labda ana mkewe nyumbani akimlea mtoto, pia, naye huko juu akimvuta, mke wa mtu mwingine? Kwa nini wanakunywa pombe? Ni kitu gani

kinachowafanya watu kutenda dhambi? Ni kwa sababu wana kiu. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁰ Mungu alipoumba moyo wa mwanadamu, alijitengenezea Mwenyewe mahali padogo mle ndani. Alikuumba ili upate kiu, sio kiu ya hilo, bali kumwonea Yeye kiu. Mwanamume ama mwanamke angethubutuje, raia wa nchi yoyote, kujaribu kutuliza hiyo kiu takatifu kwa mambo ya ulimwengu!

¹⁴¹ Hiyo ndiyo sababu wanafanya hivyo, kwa sababu, huhitaji kinywaji kingine; hamhitaji sigara, enyi wavuta sigara; hamhitaji kinywaji kingine, ninyi watu mnaokunywa pombe; huhitaji chama kingine, unamhitaji Mungu, ndiye unayehitaji, kuona kiu ya haki. Mungu alifanya mahali hapo, na kukufanya uone kiu, hiyo ni sehemu yako. Alifanya mahali hapo padogo moyoni mwako kujikalisha Mwenyewe, na kuridhisha kiu yako.

¹⁴² Haitakufaa kitu, itakufanya mraibu wa dawa za kulevya, ama—ama kitu kingine, wala kamwe hutaridhika, wala hapataridhika, mpaka utakapopata kile Kitu ambacho palifanyiziwa. Unachanganya kitu fulani tena, ukijaribu kutoa kitu pale ambacho Mungu alijitengenezea Mwenyewe. Nalo hilo, ndilo linalomfanya mtu kuona kiu.

¹⁴³ Maskini Malkia huyu, ni tofauti jinsi gani! Alikuwa akiona kiu kwa sababu maskini moyo wake mnyenyekevu ulikuwa ukimtafuta Mungu. Sasa, baada ya kitambo kidogo watu wengi sana wakaja, hata akawazia, “Vema, ninapanda kwenda kujionea mwenyewe.”

¹⁴⁴ Sasa, hilo hapo wazo zuri, angeweza kuwafundisha wanawake Wamarekani jinsi ya kuishi. Mnaona, Wamarekani watakaa nyumbani, na, “Aa, vema, Daktari *Nanii* alisema ni uongo.” Watakaa nyumbani. Mwanamke huyu hakujali yale Daktari *Nanii* aliyosema, alikuwa na kiu ya kujionea mwenyewe, naye alikuwa amekusudia kwenda. Alikuwa na mengi ya kumkabili. Kumbukeni, yeye alikuwa ni mpagani, ingembidi kwenda kumwuliza kuhani wake mpagani kama angeweza kwenda.

¹⁴⁵ Hebu na tufanye safari pamoja naye, namsikia akishuka, akisema, “Mtakatifu baba mchungaji, inawezekana kwamba ungeweza kuniwia radhi, kama Malkia? Nasikia wana uamsho mkubwa unaoendelea hapa juu katika taifa jirani, ambapo Mungu, Mungu wao ameshuka, na amewapaka hao watu mafuta, mpaka wote wako katika nia moja. Ameweka Roho Yake juu ya mtu mmoja, anaonyesha upambanuzi mkuu. Ee, baba mtakatifu, waweza kuniruhusu kutoka kanisani, ili ni niweze kwenda?”

¹⁴⁶ “Sasa, binti yangu, huna budi kukumbuka wewe ni nani, una fahari kuu. Mama yako alihudhuria kanisa hili, baba yako alihudhuria kanisa hili, babu yako, nyanya yako, na babu yao, nyanya yao walihudhuria kanisa hili. Sasa, hakuna upuuzi kama huo. Usichukuliwe na baadhi ya ulokole huo.” Mnajua watu

hufa, bali roho hazifi, kwa hiyo, zingali zinaishi, zina mitazamo ile ile.

¹⁴⁷ “Kwa hiyo usilikaribie kundi hilo, hapana shaka wao ni watakatifu wanaojiviringisha huko juu. Usiwasikilize. Sasa, kama kuna jambo lolote linaloendelea namna hiyo, lingetukia kanisani *mwetu*, unaona, lingekuwa huku chini pamoja nasi,” wangesema. “Hivyo ndivyo ingekuwa, mnaona.”

¹⁴⁸ Kwa hiyo basi, muda si muda mwajua, yeye alisema, “Lakini angalia, bwana,” hebu tusikilize yale aliyosema, “lakini angalia, bwana, yote niliyosikia juu ya nyanya yangu, na mama yangu, na kadhalika, yote hayo, ni lundo tu la kanuni za imani, na kadhalika, ambazo mnakariri hapa, mkiangalia namna fulani ya sanamu, wala hatujapata kuona tendo moja bado. Sijawahi kuona kitu ila kundi la watu wanaoishi kama walimwengu wakija hapa, na kukariri kanuni za imani, na kurudi. Wala sijaona ishara yoyote ya kimbinguni ya uhai wowote katika sanamu yoyote, wala kanisani. Nao wananiambia ya kwamba wana Makala, ya kwamba Mungu anaishi pamoja nao. Ninaenda, kwa vyovyote vile.” Amina. Ninapenda hilo.

¹⁴⁹ Ukimwacha Mungu aanze kuushughulikia moyo, hakuna makasisi wa kutosha ulimwenguni kuwazuia, wala walokole wa kutosha, kuwazuia kwake, wanakuja, kwa vyovyote vile, Mungu akianza kuushughulikia moyo wa mwanadamu.

¹⁵⁰ Ninaweza kumwona akigeuka, akitoka kanisani. Sasa, kumbukeni, kwanza kabisa yeye alikuwa ni mwanamke, maskini mama aliyepaswa kuondoka. Sasa kumbukeni, yeye alisema hivi, pia, akasema, “Sasa, ninapanda kwenda kule kujionea. Jambo la kwanza afadhali nifanye ni kununua Magombo mengi ya Kiyahudi, nione Yehova ni Mungu wa aina gani.”

¹⁵¹ Ni wazo zuri. “Mwayachunguza Maandiko, kwa kuwa ndani Yake, Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Vema.

¹⁵² Ndipo akayachunguza Magombo, na kujua yote yaliyokuwa kwenye hayo Magombo jinsi Yehova alivyokuwa, jinsi tabia Yake ilivyokuwa, yale aliyofanya. Hilo ni jambo jema kwa kila msomaji wa Biblia. Unapokuja kwenye mkutano, usielewe, angalia kama unaambatana na Maandiko, kama si wa Kimaandiko utupilie mbali, iwapo ni Maandiko, upokee. Hiyo ni kweli. Kile. . . Fanya kile Yesu alichosema ufanye.

¹⁵³ Ndipo akanunua yale Magombo, kisha akayasoma yote, akasema, “Vema, najua Magombo yanalielezea, Yeye ni wa namna hiyo, manabii wote wanasema ya kwamba Yeye ni Mu—Mungu wa namna hiyo, na Yeye ndiye Mungu wa namna hiyo. Kwa hiyo ninaenda huko juu, nami nitachukua pesa nyingi sana, endapo ni kweli, nitaiunga mkono, kama si kweli, basi sitaiunga mkono, nitarudisha pesa zangu.”

¹⁵⁴ Hilo lingekuwa somo zuri kwa Wamarekani wengi. Laiti—laiti Wamarekani wangaliunga mkono yaliyo kweli, yale

yanayothibitisha kuwa ni Mungu! Lakini karibu wanaunga mkono kila kitu ila hicho. Nadhani haina budi kuwa tu hivyo.

¹⁵⁵ Sasa kumbukeni, yeye aliwatandika ngamia wake, kisha akaondoka na wajakazi wachache, na matowashi kutoka hekaluni, naye akaanza safari yake. Sasa kumbukeni, haikumbidi kuvuka tu barabara, alikuwa na mamia ya maili kupitia Jangwa la Sahara, si katika Kadilaki iliyoyoyozwa, bali juu ya mgongo wa ngamia.

¹⁵⁶ Si ajabu Yesu alisema atasimama Siku ya Hukumu na kukihukumu kizazi hiki kuwa kimekosa, baadhi ya watu hawatavuka barabara kuona mojawapo ya hii mikutano, naye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia kusikia hekima ya Sulemani, na tazama hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani. Mungu wa Sulemani yuko pamoja nasi, hakika, akifanya jambo lile lile alilofanya katika siku za Sulemani. Si ajabu Yesu alisema atasimama katika Hukumu, na kukihukumu kizazi hiki kuwa kimekosa.

¹⁵⁷ Na jambo lingine, alikuwa na pesa nyingi, manemane, na uvumba. Loo, ilikuwa—ilikuwa, hakuna njia ya kukadiria bei yake, gharama yake ni makumi ya maelfu ya dola. Sasa ilimbidi kuvuka jangwa, watoto wa Ishmaeli walikuwa huko nje jangwani, nao walikuwa ni wanyang'anyi.

¹⁵⁸ Lakini, mnajua, kuna jambo fulani kulihusu, wakati moyo wako unapoanza kumwonea Mungu njaa, hujui hofu yoyote, unaendelea tu kusonga mbele, kwa vyovyote vile, huliwazii. “Yale Mama atakayosema, kile Papa atakachosema, kile *Fulani-wa-fulani* atakachosema, yale bosi wangu atakayosema,” unaendelea tu kusonga mbele. Unapoanza kuona njaa na kiu kwa ajili ya Mungu, kitu fulani kinaanza kuja, unakifuatilia, kwa vyovyote vile.

¹⁵⁹ Akaanza kuvuka hilo jangwa, labda ilimbidi kusafiri usiku, kwa sababu mchana ingekuwa na joto sana. Hiyo miale ya moja kwa moja ya hilo—hilo jua huko chini kwenye hilo Jangwa la Sahara karibu ingeiteteza ngozi yako kwa joto. Nanyi mnajua inachukua muda gani kuvuka, kwa msafara kuvuka jangwa hilo? Siku tisini, miezi mitatu. Lakini kulikuwa na *Kitu fulani* kilichomkokota, kikimvuta.

¹⁶⁰ Ee Mungu! Whiu! “Heri wenye njaa na kiu, maana watashibishwa.” Kuona njaa na kiu. Loo, mpaka utakapoona kiu huwezi kuelezewa hayo, bali unapoanza kuona kiu, uko tayari basi.

¹⁶¹ Alikuwa, alikuwa na... Hakuwa akiwazia kuhusu watoto wa Ishmaeli, Mungu angewalinda na hao, kama Mungu huyu alikuwa ni Mungu, Yeye angemlinda. Naye alikuwa njiani, mchana, kwenye mwangaza wa mbalamwezi... mchana angelala chini pamoja na wajakazi wake pale, na kusoma haya Magombo, na kusema, “Ni, hiyo anga kubwa, je, Yehova

aliifanya hiyo? Je, aliifanya *hii*? Nitatafuta kujua. Wanasema wana ishara pale, nitaangalia kama ni kweli.”

¹⁶² Hatimaye, akawasili kwenye malango ya ikulu. Hatimaye alipofika kwenye malango ya ikulu, hakuja tu kusema, “Nitaingia na kuketi chini, na kama jamaa huyo akisema jambo moja dhidi ya theolojia yetu kanisani mwetu, nitasimama moja kwa moja na kutoka humu jengoni kwa kishindo.” La, huo ni msimamo wa Marekani, mnaona, lakini sio wake. Alikuwa kuketi pale mpaka aliposhawishika kabisa, akiyafananisha na Maandiko. Akapiga mahema yake, na kila kitu, akajiandaa kwa ajili ya mkutano.

¹⁶³ Nami naweza kuwazia kesho yake asubuhi alijinadhifisha akavaa zilizo bora kuliko zote, na wajakazi wa—wake, nao wakaenda mlangoni. Na kwaya yote ikaimba nyimbo kuu, nazo baragumu zikapigwa, na dhabihu ikatolewa, utangulizi wote ukafanywa, ndipo Sulemani akaja jukwaani.

¹⁶⁴ Akasema, “Loo, huyo hapo. Huyo hapana shaka ndiye yule jamaa ambaye Mungu amemtia mafuta. Sasa, kama Mungu huyu. . . Sasa, hebu nione sasa, hebu nione, nitawarudia manabii hawa wote sasa, nitaona kama ni kweli.”

¹⁶⁵ Muda si muda mwajua wakaleta kisa cha kwanza, naye akaona kwamba roho ya Sulemani ya upambanuzi ilikuwa kamilifu. Siku baada ya siku, akaiangalia, hakuna dosari ndani yake, mahali popote. Maskini moyo wake ukaanza kudunda, baada ya kitambo kidogo, ulipoanza kupiga sana, hatimaye kadi yake ya maombi ikaitwa, naye akapanda juu.

¹⁶⁶ Basi alipofika pale, akasimama mbele ya Sulemani, alikuwa na siri moyoni mwake, naye Sulemani, Biblia ilisema, akamwambia mambo yote, hakuna kitu kilichofichika. Mungu akamfunulia Sulemani kila kitu ambacho alitaka kujua. Hiyo ni kweli? Hiyo ni roho ya upambanuzi, hakika, akamfunulia yote.

¹⁶⁷ Basi wakati kadi yake ya maombi ilipoitwa, naye akapanda kule juu, naye Sulemani akamfunulia jambo lote kwa Roho wa Mungu, aligeukia kusanyiko, naye akasema, “Yote ambayo nimesikia ni kweli. Na zaidi ya niliyosikia ni kweli, ni kuu kuliko nilivyowazia.” Kwa nini? Alikuwa amesimama katika Uwepo wa Yehova. Haleluya! Loo!

¹⁶⁸ Laiti ningaliweza kuleta hilo jinsi ninavyoliona. Loo, jamani! Je, mnatambua wakati Roho Mtakatifu anaposhuka, na nguvu za Mungu zinapagusa mahali hapo, Yehova yupo, Yehova yeye yule? Tunawezaje kutulia? Tufanye nini?

Mnaona, tunawazia, “Loo, laiti ningalikuwa huko nyuma wakati huo!”

¹⁶⁹ Ungejisikia vile vile unavyojisikia sasa. Ni kuu sasa kuliko ilivyo wakati huo, maana huko ilikuwa juu ya mtu mmoja, huku iko juu ya watu wote watakaompokea. Ilikuwa ni kwa ajili ya

mtu mmoja, Sulemani, sasa ni kwa yeyote atakayemruhusu aje. Amina.

¹⁷⁰ Hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani akionyesha ishara ya kufufuka Kwake. Yeye alifanyika mwili, naye akafa apate kuondoa dhambi yako, akafufuka tena siku ya tatu, akarudi katika umbo la Roho Mtakatifu, nazo kazi alizofanya, anazifanya moja kwa moja miongoni mwa watu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Haleluya! Nasema *haleluya*; maana yake ni “Mungu wetu asifiwe.” Loo, naam. Yuko hapa.

¹⁷¹ Si ajabu Yesu alisema, “Atafufuka katika Siku ya Hukumu na kukihukumu hiki kiza-...” Isitoshe, angalia kile alichouambia Shreveport, na hizi sehemu zingine nyingi, makanisa ya Kipentekoste: “Isitoshe, bali heri wale walio pamoja nawe, wanaosimama na kuhudumu pamoja nawe. Heri wao, kwa kuwa wanaona mambo haya yakitendeka siku baada ya siku, heri wao. Heri watu walio pamoja nawe, wanaosimama karibu nawe, wanaoona karama hii ikitenda kazi siku baada ya siku.”

¹⁷² Yesu alisema atasimama katika Hukumu na kukihukumu kizazi hicho, hiyo ni kweli, na kukihukumu kizazi *hiki*. Ni zaidi sana jinsi gani yeye atakihukumu *hiki* kuliko *kile*? Kwa sababu angalieni hii Nuru kuu zaidi sana tuliyo nayo tangu siku hiyo: mauti, kuzikwa, kufufuka, Roho Mtakatifu Mwenyewe papa hapa pamoja nasi. Mnaona ninalomaanisha? Ni wa kawaida sana. Hivyo ndivyo—hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo kwa Wapentekoste, ni wa kawaida sana.

¹⁷³ Mzee mmoja wakati mmoja aliyeishi huko barani, alikuwa akienda zake ufukoni mwa bahari. Naye angeandika vitabu, na mara nyingi alikuwa ameandika juu ya bahari, jinsi ilivyokuwa nzuri. Siku moja akishuka kwenda zake, alishuka kwenda ufukoni mwa bahari, naye akakutana na maskini baharia akitoka baharini, naye akasema, “Unaenda wapi, mtu wangu mwema?”

¹⁷⁴ Akasema, “Loo, ninaenda baharini! Sijawahi kuiona maishani mwangu.” Naye akasema, “Ninataka kuona mawimbi yake makubwa, meupe, ya chumvi yanapopiga kwa nguvu; ninataka kuinusa harufu ya hewa ya chumvi; ninataka kusikia kilio cha shakwe wa baharini.”

¹⁷⁵ Yule baharia mzee akasimama pale, akaangalia, akatafuna shina la kiko chake kidogo, akasema, “Nilizaliwa juu yake, nimekuwa juu yake kwa muda wa miaka hamsini, sioni cha kusisimua sana juu yake,” kisha akaenda zake. Jambo ndilo hilo, alikuwa ameizoea sana, haikumsisimua, tena.

¹⁷⁶ Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, mmeona mengi sana Yake, haliwasisimui, tena. Roho Mtakatifu ni mwema sana kuwatembelea wakati baada ya wakati, baada ya wakati, baada ya wakati, nasi tunamsahau.

¹⁷⁷ Huko Louisville, Kentucky, majuma machache yaliyopita kulikuwa na mama aliyekuwa amembeba mtoto mchanga, naye, akitembea pale, naye alikuwa akitikisa wanasesere wadogo, mwajua, akisema, “Unaona, Kipenzi? Unaona, Kipenzi?” Halafu angechukua kitu kingine, “Unaona, Kipenzi? Unaona, Kipenzi?” Maskini mtoto huyo mchanga aliendelea tu kukodoa macho.

¹⁷⁸ Ndipo baada ya kitambo kidogo li—likawasumbua watu dukani. Hatimaye, akachukua kengele ndogo iliyolia, akasema, “Angalia, Mpenzi! Angalia, angalia, angalia, angalia! Kipenzi cha mama, angalia!” Naye maskini mtoto huyo mchanga akakodoa macho tu, naye mama akaanguka kwenye kaunta.

Ndipo watu wakaja kumsaidia, wakasema, “Kwani kuna shida gani?”

¹⁷⁹ Akasema, “Loo, mvulana wangu mdogo, hapa si muda mrefu uliopita,” kasema, “alianza tu kukodoa macho moja kwa moja angani.” Kisha kasema, “Nilimpeleka kwa daktari muda mfupi uliopita, naye akasema amepata nafuu, lakini sivyo.” Kasema, “Hakuna kitu kitakachomvutia.” Kasema, “Mambo yanayopaswa kumvutia mvulana mdogo wa umri wake, hayamvutii, yeye huketi tu na kukodoa macho angani.”

¹⁸⁰ Jinsi hilo lilivyo kweli kwa kanisa leo hii! Mungu alitikisa karama ya kila namna awezayo mbele ya kanisa, nao wangali wanaketi na kukodoa macho, wakitafuta kitu kingine. Haleluya! Hiyo ni kweli. Mungu atachoka, kuzitikisa karama mbele yenu baada ya kitambo kidogo. Mnaketi mumpooza.

¹⁸¹ Mnamwona Oral Roberts fulani, na kadhalika, akiwaponya wagonjwa, na ishara kuu na maajabu ya Masihi aliyefufuka, nao watu wanaketi, wanasema, “Vema, sijui.” Mnaona?

¹⁸² Haiwavutii tena, akili zao zimepatwa na jambo fulani. Wanaonekana tu kama wamechanganyikiwa tu kiakili, ama wamevurugika kiroho. Na tabia yao, unaweza kuwaambia kuhusu utakatifu, na jinsi ya kuishi, hawatilii maanani hilo zaidi, kana kwamba hata hukulisema. Haininii . . . Hawatambui ya kwamba mwana na binti ya Mungu wanapaswa kutenda kama mwana na binti ya Mungu, wanapaswa kutambua mahali pao, sio kuzozana, kupigana, kugombana, kufanya yasiyofaa, kuwa na kinyongo.

¹⁸³ Hapa wakati fulani uliopita hapa kusini, walikuwa wakiwauza watu weusi kama watumwa. Nao wangewauza uwanjani, kama tu vile ungeuza magari, magari ya mitumba, upate hati ya mauzo nao. Kamwe halikuwa sawa. Ndipo wakati . . . Siku moja akaja dalali, naye alitaka kununua watumwa kwenye shamba fulani. Nao wangewanunua wanaume wakubwa na kuwazalisha kwa wanawake wakubwa, wapate kuzaa watumwa wazito zaidi wa kuvuta mikokoteni yao, na plau, na kadhalika, na kufanya kazi yao. Basi siku moja dalali akaja, naye akasema, “Una watumwa wangapi?”

Kasema, “Nina mia moja, ama mbili.” Kasema, “Waangalie.”

¹⁸⁴ Akawaona wote, walikuwa mbali na nchi za uenyeji wao, nao iliwabidi kuwapiga mijeledi, na kila kitu, kuwafanya watii, na, kwa sababu walikuwa na huzuni, walijua hawangerudi nyumbani tena, ingewabidi kufia hapa katika nchi ya kigeni, wala kamwe hawangerudi nyumbani tena.

¹⁸⁵ Lakini walimwona kijana mwanamume mmoja, haikuwalazimu kumcharaza, jamani, alikuwa kifua mbele, kidevu juu, sikuzote alikuwa chonjo. Huyu dalali akasema, “Ningetaka kumnunua mtumwa yule.”

Akasema, “Lakini yeye hauzwi.”

Kasema, “Kwa nini hauzwi?” Kasema, “Kwani yeye ndiye bosi wa hao wengine?”

Kasema, “La, yeye ni mtumwa.”

Kasema, “Je, unamlisha tofauti na unavyowalisha hao wengine?”

Kasema, “Wote wanakula kwenye manchani, pamoja.”

Kasema, “Ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na hao watumwa wengine?”

¹⁸⁶ Ndipo mwenyewe akasema, “Hilo lalinishangaza kwa muda mrefu, lakini siku moja nilipata kujua. Huko kwenye nchi ya uenyeji wake, alikotoka Afrika, baba yake ndiye Mfalme juu ya hilo kabila. Na ingawa yeye ni mgeni, na yuko mbali na nchi ya uenyeji wake, angali anaenenda kama mwana wa Mfalme.”

¹⁸⁷ Hmm! Tunapaswa kuenenda namna gani? Kama waoga? Sisi ni wana na binti za Mungu! Sisi ni wageni, sisi ni wasafiri na wageni hapa, bali tunatembea tena juu ya Neno la Mungu. Ni ninii Yake. . . Sisi ni wana na binti za Mfalme, hatutasema uongo, kuiba, kunywa pombe, kuvuta sigara, kufanya vituko vya namna hiyo, wanawake hawapaswi kukata nywele zao na kutenda kama wanawake wa mitaani, kuvaa nguo kama hizo, sisi ni wana na binti za Mungu, wana wa Mfalme na binti za Mfalme. Hii si nchi yetu, tutakufa katika nchi hii siku moja, bali tuko njiani mwetu kwenda Nyumbani. Hebu na tuenende kama wana na binti za Mungu. Hiyo ni kweli.

Basi *malkia wa kusini atasimama . . . siku ya hukumu*, naye *atakihukumu kizazi hiki kwamba kimekosa*; kwa sababu *alikuja kutoka pande za mwisho za dunia aisikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani*.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

Mimi ni mtoto wa Mfalme!

Mimi ni mtoto wa Mfalme!

Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,

Mimi ni mtoto wa Mfalme!

Baba yangu ni tajiri wa nyumba na mashamba,
Yeye anaushikilia utajiri wa ulimwengu
mikononi Mwake!

Wa rubi na almasi, wa fedha na dhahabu,
Makasha yake yamejaa, Ana utajiri
usiosemeka.

Mimi ni mtoto wa Mfalme!
Mtoto wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mtoto wa Mfalme!

¹⁸⁸ Kama wewe si mtoto wa Mfalme na ungetaka kuwa usiku wa leo kuja ujiunge na safu katika Mwili wa kisiri wa Kristo, na kumpokea kama Mwokozi binafsi, ujazwe na Roho, waweza kuinua mikono yako, na kusema, “Niombee Ndugu Branham”?

¹⁸⁹ Sina wakati wa kufanya wito wa madhabahuni hapa, nataka tu kujua kama mnetaka niwaombee. Mungu akubariki, bwana. Mungu awabariki, kote jengoni. Mungu awabariki. Mikono mingi, dazani moja ama mbili, iliinuliwa. Mara nyingine sasa wakati Roho Mtakatifu akilizamisha ndani ya kilindi cha moyo wao:

Mimi ni mtoto wa Mfalme!
Mtoto wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mtoto wa Mfalme!

¹⁹⁰ Baba Mungu, ni Wewe uliyesema Malkia wa Kusini atasimama, na katika nukuu hii ya mwisho ambayo ingekihukumu kizazi hiki, na Yona, kizazi kiovu na kinachotafuta ishara. Tunao siku hizi, Baba, kamwe hawataliamini jinsi ulivyoliandika, wanasema, “Hebu nikuone ukifanya jambo fulani. Nionyeshe muujiza. Nionyeshe *hili*.” Hawatambui ya kwamba roho iliyo ndani yao imekuwako katika nyakati zote ndani ya watu.

Walimwambia Bwana wetu, “Utuonyeshe ishara, tunatafuta ishara.”

Yeye akasema, “Kizazi hiki chote kiovu kitapokea ishara, ishara ya ufufuo.”

¹⁹¹ Tuna furaha sana usiku wa leo. Na ishara ile aliyokuwa akinena habari zake wakati huo juu ya Yona, kitu kile kile walichosema alikuwa Beelzebuli, kwa sababu angeweza kuyatambua mawazo ya moyo wao, mlango uo huo ulisema Yeye alijua mawazo moyoni mwao, nao wakasema Yeye alikuwa ni ibilisi. Naye akawaambia jinsi Malkia wa Kusini alivyokuja kutoka huko mbali Sheba kusikia he—hekima ya Sulemani, na aliye mkuu kuliko Sulemani alikuwa hapo.

¹⁹² Na sasa, leo Bwana Yesu yeye yule aliyefufuka yuko miongoni mwetu, katika umbo la Roho Mtakatifu, pamoja nasi

hapa, akitenda kazi ndani yetu, akifanya mambo yale yale. Na kizazi kiovu, kizazi cha zinaa, kuoa, kuolewa, mahakama za talaka, upotovu, upotovu wa zinaa, uovu wa kila namna: “Tuonyeshe ishara.” Unaionyesha, ufufuo, bali hawataiamini, Baba.

¹⁹³ Sasa, hawa waliomo humu ndani, na kama nilivyosema kuhusu huyo—huyo mtumwa mweusi, jinsi ambavyo haikumbidi kucharazwa, la, haidhuru alikuwa na magumu jinsi gani, angali alijua alikuwa m—mwana wa Mfalme, aliuchochea uadilifu wa hao wengine kwa tabia yake mwenyewe, na, Baba, hebu sisi, kama Wakristo, wale walio na nguvu katika Kristo, tutende kama watoto wa Mungu, tuzungumze kama watoto wa Mungu, tukiwa na hakika juu ya Neno la Mungu, tukijua yale Roho Mtakatifu ametufanyia.

¹⁹⁴ Mikono mingi iliinuliwa, kwamba walitaka kumpokea kama Mwokozi binafsi na kuwa mtoto Wake. Mungu, ninaomba ya kwamba katika mstari huu wa maombi, mahali fulani, pale, ama, mahali fulani mkutanoni, ya kwamba Wewe utaonyesha ishara hiyo ya ufufuo uliyohidi kupitia kwa Yona. Na jalia saa hiyo, ama, wakati huo, jalia nguvu za Mungu ziwatie muhuri moyoni mwao kwa Roho Mtakatifu na kuwafanya wana na binti za Mungu, ili tabia zao zibadilishwe, shauku zao, na malengo yao, na nia, na kila kitu maishani mwao kingebadilishwa. Tujalie, Bwana.

¹⁹⁵ Tunakungojea Wewe zaidi, ibada ni Yako, iko katika Jina Lako, nasi tunangojea kuona utakalofanya. Waokoe hawa Bwana, usiwaache waondoke kwenye jengo hili, usiku wa leo bila wokovu. Tujalie, Bwana.

¹⁹⁶ Jalia wote wajazwe na Roho Mtakatifu. Na jalia huu uwe ndio upeo wa maisha yao, sasa hivi, kwamba wataondoka kwenye jengo hili usiku wa leo, na wengine wengi ambao hawakuinua mikono yao, wakishangilia, wakisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu? Nasi tunajua ya kwamba Yesu amefufuka katika wafu, kwa sababu tulimwona akiwaponya wagonjwa, na kufanya yale hasa aliyosema angefanya katika siku za mwisho. Tunampokea kwa unyenyekevu.” Tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

Pamoja na Yesu Mwokozi wetu,
Loo, sisi ni watoto wa Mfalme!

Mnaweza kuinua mikono yenu, na kuuimba pamoja nami mara moja?

Mimi ni mtoto wa Mfalme!
Mtoto wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mtoto wa Mfalme!

Hivi huna furaha?

Yule Tabibu mkuu sasa yuko karibu,
 Yesu mwenye huruma;
 Yeye huunenea ninii uliohuzunika . . . ,
 Loo, isikieni Sauti . . . Yesu,
 Sauti tamu sana . . . wimbo wa maserafi,
 Jina tamu kuliko yote kwenye ninii wa
 mwanadamu . . . ,
 Wimbo mzuri sana uliowahi kuimbwa,
 Ni Yesu, Yesu mbarikiwa.

Yeye si ni wa ajabu? Sasa kwa uchaji, kila mtu. Na sasa, muziki, kama utaendelea na huo, Dada Anna Jeanne.

197 Ninaamini Paul aliniambia, ninaamini uligawa kadi hamsini, sivyo, Bill? Kadi za maombi B, tukizichukua za zamani, na kuwapa zile mpya, nisije nikachanganyikiwa.

198 Sasa, kadi hamsini za maombi, sasa usiku wa leo hatutaanza, tutawaombea tu wagonjwa. Tunaamini ya kwamba katika mstari huu wa maombi . . . Ninataka kuwaombea wote, ninataka kila mtu aombewe. Na kwa hiyo, sasa tutawaita watu hao hapa juu.

199 Kadi ya maombi . . . Ninapoita namba yako, utasimama? Ili kwamba kama kuna mtu tunayepaswa kumsaidia, mbona, tunaweza kuwaingiza mstarini. Kadi ya maombi namba moja, ni nani aliye nayo? Una hakika ulikuwa sahihi? Kadi ya maombi namba moja? Ni—ni herufi gani? B, namba moja. Unayo, mama? Shuka moja kwa moja hapa chini. (Chukua kiti na uketi pale chini, Billy, kwa ajili ya . . .)

200 Namba mbili. Ni nani aliye na kadi ya pili ya maombi, waweza kuinua mkono wako? Mama huyu hapa. Namba tatu. Nisaidieni, mtu fulani, Ndugu Palmer, angalia mkono wao. Inua mkono wako ukiweza, ninapoita namba yako. Namba tatu. Mtu huyu hapa. Namba nne, namba tano. Njoo tu moja kwa moja huku, chukua tu nafasi yako. Namba sita, namba saba, namba nane, tisa, kumi.

201 Kwa kawaida, kama tutakuwa na mstari wa upambanuzi, sikuzote mimi hujaribu kuruka tu na kuanzia ishirini, au thelathini, ama mahali fulani namna hiyo, lakini kwa njia hii haileti tofauti yoyote, maana tuta—tutaomba moja kwa moja mstarini, maana nitajaribu kuwaombea wote.

202 Kumi, kumi na moja. Nisaidieni sasa. Kadi ya maombi kumi na moja, kumi na moja. Mmeipata? Kumi na mbili. (Angalieni hapo.) Kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na tano. Vema. Kumi na sita, kumi na saba. Hapana shaka mtu fulani aliichukua akaenda nyumbani. Wasemaje? Karibu upande huu? Vema, tutaanzia papa hapa basi. Isogeze moja kwa moja . . . Huh? Loo, naam. Kumi na saba, vema, papa hapa. Ni nani aliye na kumi na saba? Hakuna mtu?

Kumbukeni niliita. Kumi na nane, kumi na tisa, ishirini, ishirini na moja.

²⁰³ Simama tu papa hapa mpaka awe tayari kwa ajili yako, aje moja kwa moja humu ndani. Ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano, ishirini na sita, ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini na tisa, thelathini. Sikuona thelathini. Kadi ya maombi thelathini. Thelathini. Mnaiona? Kila mtu huzungumza Kiingereza hapa, nadhani, Kifaransa au Kiingereza.

²⁰⁴ Kuna mtu anayejua kama kuna mtu anayezungumza Kifaransa, ama chochote kile? Thelathini, thelathini. loo, unayo? Loo, sikuona, samahani. Thelathini na moja, thelathini na mbili, thelathini na moja, thelathini na moja, thelathini na mbili. Jambo ndilo hilo. Thelathini na tatu. Hiyo ndiyo njia. Thelathini na tatu, thelathini na nne, thelathini na tano, thelathini na sita, thelathini na saba, thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini.

²⁰⁵ Jambo ndilo hilo, fanyeni mstari papa hapa. Mnaona? Njoni huku kila mtu sasa, mkipitia pale. Mnaona? Kama ukiondoka . . . Vema, arobaini, arobaini na moja, arobaini na mbili, arobaini na tatu, arobaini na nne, arobaini na tano, arobaini na sita. Hamkuiona, sivyo? Arobaini na sita, naam, arobaini na sita, arobaini na saba, arobaini na saba, arobaini na nane. Vema. Arobaini na tisa, hamsini, hamsini. Je, niliiona? Hamsini, hamsini. Hiyo ni . . . ? Hao walikuwa ndio wote, sivyo? Vema. Bila shaka.

²⁰⁶ Vema, sasa, wakati wakipanga mstari huku wakiita majina ya—yao, na kuwapanga katika—katika . . . ikiwa mtu angewasaidia kule chini kuwapanga watu. Huu ni mstari mrefu wa maombi, tutachukua tu wakati wetu, na kumwombea kila mtu. Sasa, sasa iweni na kicho sana kila mtu wakati wakipanga mistari ya maombi.

²⁰⁷ Sasa ningependa kuwaambia jambo hili: Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba hakuna mtu anayeweza kukuponya? Ni wangapi wanaojua ya kwamba uponyaji ni, uponyaji wa Kiungu ni kazi ya Mungu iliyomalizika pale Kalvari? Mnaona? Imewekwa msingi juu ya “atakaye na aje, na akubali uponyaji wao kwa imani,” uliamini. Hiyo ni kweli? Kwa imani unaliimini.

²⁰⁸ Sasa, watu wengine wana karama, kama mhubiri mzuri kweli, anaweza kufanya, kuchukua hilo Neno la Mungu, na kuliweka tu hapo namna *hiyo*, mwanatheolojia mzuri, na anaweza, hiyo ni karama ya uponyaji, wanaweza kuwafanya mlione kupitia kwa Neno. Sasa, siwezi kufanya hivyo, kwa sababu mimi—mimi si mhubiri sana.

²⁰⁹ Kwa hiyo, basi si—siwezi kuifanya hivyo. Mungu aliona kutokujua kwangu hilo, kwa hiyo basi akanipa njia nyingine ya kuwafanya mlione, Yeye alinipa karama ya kudhihirisha ufufuo

wa Mwanawe Yesu, kupitia *hiyo* mpate kuamini. Hiyo ni njia nzuri, sivyo? Kumwamini Mwana wa Mungu. Hiyo si ni kweli? Ndipo unapofanya hivyo, basi uta—uta—utaponywa. Sasa, kama anaweza kuthibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa. . . Wangapi wanaelewa hilo sasa? Hebu tuone.

²¹⁰ Ninatazamia tu jambo fulani kutukia katika mstari huu wa maombi, usiku wa leo, sijui ni kwa nini, uh-uh. Ninaninii tu—ninajisikia vizuri sana, kwamba ni—ninahisi kwamba—kwamba jambo fulani litatukia.

²¹¹ Naam, watu ambao ni walemavu, ama chochote kile, wawekeni tu moja kwa moja hapa, kama vile viti, na kadhalika, nita—nitashuka, niwaombee, bwana.

²¹² Ninataka kuweka hivi hapa juu, ninapenda kuhisi upako wa Roho kwanza, kabla si—sijaombea vitambaa hivi na kadhalika. Sasa, ninawatakeni mwe na kicho kabisa. Na kuninii tu, sasa, sininii. . . Ninapomaanisha kicho. . . Mnaona, wakati Roho Mtakatifu anaponena. . .

²¹³ Sasa, watu hawa wote katika mstari huu wa maombi hatufahamiani, si—sioni mtu hapo ninayemjua. Ndugu Babbs yuko hapo? Naam, Ndugu Babbs yuko huko nyuma, ninamfahamu. Nadhani, mnamwona mtu yeyote humo ndani ninayemjua? Mama mmoja anatikisa kichwa chake pale kwamba nilimjua, kwa hiyo mimi. . . Je, ninakujua hapo, mama? Mimi. . . Loo, nilikuombea. Ninamaanisha, mimi. . . Vema, ninajua hili: sijui una tatizo gani. Sina wazo la kujua shida yako, hakika. Lakini Mungu anajua, sivyo? Kwa hiyo hilo ndilo tunalowazia.

²¹⁴ Sasa, katika kusanyiko, nadhani kadi zote za maombi zimesimama hapa mstarini, wewe katika kusanyiko usiye na kadi ya maombi, na hata hivyo unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na kukupa afya, ni wangapi wanaoamini hilo? Sasa, Mungu na atujalie.

²¹⁵ Sasa, hebu na tusiwe na haraka, kila mtu awe na kicho. Sasa, kwa mstari huu wa maombi, labda itachukua kama dakika ishirini kumaliza mstari wa maombi. Na ndipo tukifanya hivyo, sitaki kuwapitisha tu kwa kuwawekea mikono, ninataka kuwaombea. Nita. . . Ni—ni—ninaamini ya kwamba hiyo ndiyo njia kama mimi, Mungu ataniruhusu kufanya hivyo. Lakini ninawatakeni mjue sasa, bila upambanuzi wowote, Roho Mtakatifu yupo hapa, kwa vyovyote vile.

²¹⁶ Hapa si muda mrefu uliopita kulikuwa na mtu katika mkutano fulani ambaye kamwe hakuamini mafundisho yangu juu ya Biblia. Naye akaenda kwenye mkutano, jamaa fulani alifanya hivyo, na bila kujua kwamba ninajua habari zake, maana mara tu alipolisema, nami ningeliona katika ono katika chumba changu cha hoteli. Sioni jinsi watu wengine wanavyoweza kufanya hivyo, na kuja, na kusema mambo haya, wakati unajua unafahamu vizuri zaidi. Mnaona?

217 Kwa hiyo, akasema, “Sasa, Ndugu Branham ni nabii wa Bwana,” akasema, “lakini msiyasikilize mafundisho yake, kwa sababu yuko makosani.”

218 Roho Mtakatifu yeye yule aliyehubiri ibada usiku wa leo, Roho Mtakatifu yeye yule anayehubiri mambo haya yote, ndiye Roho Mtakatifu yeye yule anayeyatambua mawazo ya moyo. Bila shaka.

219 Alama ya nabii ni nini? Yeye ni mfasiri wa Kiungu wa Neno la Kiungu. Hiyo ni hakika. “Neno la Bwana lilimjia nabii.” Huyo ndiye lililomjia, si mwanatheolojia, nabii. Mnajua maana ya *nabii*? Chukua kamusi uangalie uone maana yake: “Mfasiri wa Neno la Kiungu.”

220 Na kisha uje na kusema kitu kama hicho! Mnaona jinsi...? Watu wamekuwa wa *kanisa* sana, hata hawamjui Mungu tena. Jambo ndilo hilo. Hilo ndilo linalotufanya tuwe wa *kinyumbu* sana. Uh-huh. Ni ninii tu, unataka kurudi kwenye hatua hiyo ya imani halisi, ya kweli ya Roho Mtakatifu.

221 Naam, ninamwona mtu mmoja ninayemjua, huyu ndugu Mbaptisti aliyeketi hapa, Ndugu Daulton. Ninataka kusema jambo fulani. Ninatarajia, Ndugu Daulton...Mnaona kile ninawachopangia huko juu.

222 Ni wangapi waliosikia hadithi ya kuchakulo na kadhalika? Nyote mliisikia huku chini, nadhani, na kadhalika. Huduma mpya inaimarika maishani mwangu, hiyo ndiyo sababu nina hizi hapa usiku wa leo kuzijaribu. Niliona likitukia yapata mara tatu ama nne. Mara ya kwanza lilipopata kutukia, kwa mwanadamu; mara ya pili lilipotukia ilikuwa ni kwa huyu ndugu Mbaptisti aliyeketi hapa. Yeye amesimama pale kanisani, watoto wake matineja, wazembe wawezavyo kuwa. Naye alikuwa, tulikuwa tukiwaombea watoto wake, mara Yehova-Yire yeye yule akageuka, nikasema, “Ninakupa watoto wako, katika Jina la Yesu Kristo.”

223 Nafikiri kila mmoja wao ameokoka sasa, kila mmoja wao, wote wameokoka, kila mmoja wao. Ndugu aliyeketi papo hapo kutoka Willow Shade, ama Somerset, si ni Kentu-..., Somerset, Kentucky. Mtu fulani humu ndani, baadhi yenu ninyi Wabaptisti mnataka kumwona mhubiri wa Kibaptisti aliye na Roho Mtakatifu? Simama kwa dakika moja tu, Ndugu Daulton. Huyo hapo mhubiri wa Kibaptisti wa Kentucky aliye na Roho Mtakatifu. Si ni ajabu? Ndivyo hakika.

224 Vema. Sasa hebu tuwe na kicho kabisa. Ndugu Brown, hivi wewe...? Ama, baadhi yenu msaidie kutoka upande huu wa jukwaa. Sasa ninyi msio na kadi za maombi, iweni na kicho kabisa, tulieni tu kabisa sasa, kila mtu. Sasa, kama Bwana akifanya jambo fulani, nawe unataka kumsifu, vema, lakini, mnaona, tulia tu mahali pako, endeleeni kungojea, endeleeni

kuwa na matarajio. Ninyi mlio huko nje sasa, msio na kadi ya maombi, labda Roho Mtakatifu angesema, “Geuka.”

225 Ni wangapi hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hii hapo kabla? Hebu tuone mikono yenu. Kamwe hukuwa katika... Vema, jamani, jamani! Nadhani ni... Mngali mnaelewa huu mkutano, huduma yangu? Ni, hamjawahi kuwa katika mmoja, lakini hata hivyo mnalielewa? Inueni mikono yenu. Vema, hilo—hilo ni sawa basi, ha—hamjaninii... Mnaelewa.

226 Mnaona, si mimi, bali Yesu, Mwana wa Mungu, ndiye Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, kukiri, jambo lile lile, ameketi mkono wa kuume wa ukuu wa Mungu, ameketi pale, akifanya maombezi juu ya kukiri kwetu. Hiyo ni kweli? Kwanza, inatubidi kukiri Yeye amefanya hivyo, ndipo anaanza kufanya maombezi.

227 Naye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na nini? Mambo ya udhaifu wetu. Basi kama tunaweza kumgusa kwa mambo ya udhaifu wetu, Naye ni Kuhani Mkuu yeye yule jana, leo, na hata milele, si angetenda vivyo hivyo? Hiyo ni kweli? Basi alifanyaje wakati mwanamke alipomgusa? Aligeuka, akamwambia kuhusu kutokwa kwake na damu, na kumwambia imani yake ilikuwa imemwoko. Hiyo ni kweli?

228 Ni wangapi huko nje mnaowazia mnayo, ambao ni wagonjwa wanaowazia una imani ya kutosha kumgusa Yeye, hebu tuone mikono yenu, kila mahali, kwamba u mgonjwa. Mungu awabariki.

229 Ni—ninaamini, hebu, vema, hebu tu tumchukue mmoja, kusudi tuweze kuanza, huo upako. Kama ni mtu mmoja tu, nyote hamtasema chochote, endeleeni tu. Hiyo ni kweli? Ninataka kupata upako kwanza, kusudi watu watambue.

Mwanamke huyu hapa, nadhani hatufahamiani, sivyo, mama? Hatufahamiani.

230 Vema. Huyu hapa mama ambaye hatufahamiani. Tulizaliwa umbali wa maili nyingi, miaka mbalimbali, na hii ndiyo mara yetu ya kwanza tuliropata kukutana maishani, ni juavyo mimi. Anasema yeye ni mgeni, na Mungu anajua simjui. Kuna kitu kilichomleta huyu mwanamke hapa, huenda ikawa ni tatizo la kinyumbani, huenda ikawa ni tatizo la kifedha, huenda ikawa ni ugonjwa, huenda ikawa ni kwa ajili ya mtu mwingine, sijui.

231 Lakini hii ni ishara, kama Yohana Mtakatifu 4, kulifanya la Kimaandiko kwenu, mwanamke na mwanamume wakikutana kwa mara yao ya kwanza duniani. Yesu alizungumza na mwanamke kwa dakika chache tu apate kujua, kuishika roho yake. Ni wangapi wanaojua hilo? Alianza kuzungumza naye kuhusu ubaguzi, akasema, “Si vema kwenu kuniomba mimi Msamaria, bali, kuwa na uhusiano wowote sisi kwa sisi.”

Lakini alipoona shida yake, Yeye alisema, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.” Naye akamwambia.

²³² Naye akasema, “Mimi, Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii. Sasa, tunajua ya kwamba ajapo Masihi, aitwaye Kristo, wakati Yeye, tunajua Yeye yuaja, atakapokuja hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake.”

²³³ Ni wangapi wanaojua jambo hilo, Biblia inafundisha jambo hilo? Vema, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, si ingekuwa ni ishara ile ile leo? Sisi hapa, wawili pamoja, hatujawahi kukutana hapo kabla.

²³⁴ Sasa, kama Yeye atamwambia yaliyokuwako, sasa, yeye atajua kama ni kweli ama si kweli, shida yake, ama kilichomleta hapa, jambo nisilojua, lolote lile, basi atajua kama ni kweli ama si kweli, basi hakika, angejua jambo hilo, kila mtu ingembidi kujua lingetokana na nguvu fulani za kiroho. Hiyo ni kweli? Kwa sababu hakuna njia kwangu kumjua huyu mwanamke, sijawahi kumwona, yeye hanihui, nasi hapa tumesimama.

²³⁵ Nanyi huko nje, siwajui, bali Mungu anawajua, Naye aliahidi kufanya jambo hili. Hafanyi hivi kwa sababu Yeye—Yeye anataka tu kukuonyesha wema Wake, Yeye anafanya hivyo ili kutimiza Neno Lake. Yesu aliwaponya wagonjwa, si kwa sababu ilimbidi kuwaponya, bali kwa sababu alitaka kulitimiza Neno. Hiyo ni kweli kabisa, hiyo ndiyo sababu Yeye alifanya hivyo, “ili litimie neno lililonenwa na nabii.” Na hili ni, lipate kutimizwa lililonenwa na Yesu, ya kwamba angefanya hivyo katika siku hizi za mwisho.

²³⁶ Loo, inatupasa kulibomoa jengo, inaonekana, kwa furaha. Mnaona? Lakini tungali tunazitikisa hizo kengele ndogo, na kukodoa macho, mnaona.

²³⁷ Loo, utukufu! Hmm! Hilo tu, *hilo* linapotokea, mnalihisi, ni *kitu fulani* tu, sijui.

Unasema, “Hujisikii hivyo.”

Unafikiri tu sijisikii, hakika najisikia.

²³⁸ Vema, dada, neno moja tu nawe, nizungumze nawe kwa dakika moja tu. Moja ya siku hizi tutakutana na Mungu, itatubidi kuwajibikia mambo yote ambayo tumewahi kufanya maishani. Kama Bwana Mungu atanifunulia jambo fulani lililokuleta hapa, ama *jambo lingine* maishani mwako, vema, utajua kama ni kweli ama si kweli, sivyo? Na basi kama akifanya hivyo, utaamini basi? Unajua nisingeweza kufanya hivyo, kwa sababu sikujui, endapo Yeye atafanya hivyo, basi utaamini ni nguvu Zake, Roho Wake anayefanya jambo hilo? Hakika ungeamini, hilo ni sawa.

²³⁹ Ninafanya hivi, angalau ku—ku—kuishika roho yake. Hiyo ni kweli kabisa. Tuko hapa, wanadamu wawili, na hii ni mara ya

kwanza kukutana, nawe ni roho, nami ni roho, Roho Mtakatifu yuko hapa akijaribu kuona hilo tatizo.

²⁴⁰ Naam, bwana, ninaona tatizo la huyu mwanamke. Ana kansa, nayo hiyo kansa iko kwenye mkono wako uliofunika, nisije nikaiona, bali Yeye anaijua. Hiyo ni kweli. Vema, bwana. Una shinikizo kuu la damu, magonjwa ya ziada. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Sasa, unaamini? [Dada huyo anasema, “Hakika.”—Mh.] Basi ninayakemea maradhi yako yote, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina. Nenda nyumbani, na uwe mzima sasa, Yesu Kristo anakuponya.

²⁴¹ Hatufahamiani na mwanamke huyu. Tulizaliwa, labda, umbali wa maili kadhaa, na wa miaka kadhaa. Yeye ni mdogo sana wa umri kuliko mimi, na hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukuta-... Vema, ngoja sikupaswa kuwa na upambanuzi huo, bali nilikuwa tu niendele, lakini, vema, nilianza, afadhali niendele na... Vema.

²⁴² Sasa, mama, kama nitaweza, kwa njia ya Roho Mtakatifu, kukwambia jambo fulani kukuhusu, jambo ambalo unajua kwamba silijui, basi ungenikubali kama mtumishi Wake, na kuamini ya kwamba Roho huyo ni Kristo, Mwana wa Mungu? Ungeamini hilo?

²⁴³ Kwa kweli si wewe, ni mtu mwingine, ni mwanamke mkongwe, ni mama yako, ana uvimbe. Nami ninakuona ukiangalia kwenye dirisha la maonyesho, mahali fulani, nimepaona hapo kabla, panaonekana, ni Arkansas, Fort Smith. Mama yako amekuwa kwenye mikutano yangu mahali fulani, aliponywa hapo awali. Hiyo ni kweli.

²⁴⁴ Mumeo ana shida na macho yake, sivyo? Ameketi hapa nje. Yeye atakuwa mzima sasa. Wewe ni Bibi Medcalf. Sasa, wewe rudi tu, mwamini Bwana Yesu Kristo, na uponywe.

Baadhi yenu huko nje msio na kadi ya maombi sasa, amini kwa moyo wako wote. Mnaamini?

²⁴⁵ Mama mkongwe, huna kadi ya maombi, bila shaka huna. Kama... Siwezi kukuponya, mama. Ni binti yako. Unaamini ya kwamba Mungu atanifunulia shida yako? Utalikubali? Ni ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Uponywe, katika Jina la Yesu. Nenda nyumbani ukaupokee. Mwamini Mungu. Usiwe na shaka, amini mambo yote.

²⁴⁶ Mtu huyo aliyeketi huko nje akiwa na fistula, unaamini Yesu Kristo atakuponya, kama unaweza kulikubali? Vema, bwana, inua mkono wako, uliyevaa shati jeupe. Kwa namna fulani ulishangaa una imani nyingi hivi, sivyo?

Mama aliyeketi kule nyuma, mwenye kofia ndogo, unaumwa na kichwa, sivyo, dada? Kipandauso. Mwamini Mungu, Mungu atakuponya.

²⁴⁷ Sasa, unaona, si lazima uwe hapa juu, inakubidi kumwamini Mungu. Hiyo si ni kweli? Mwamini Mungu, hivyo tu. Unaamini kwa moyo wako wote? Usitie shaka, amini, uwe na imani, mwamini Mungu.

²⁴⁸ Simjui mtu huyu, hatufahamiani. Hiyo ni kweli, bwana? Kama Mungu atanifunulia shida zako, je, utaniamini kama mtumishi Wake, umwamini Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu? Utaamini? Una pumu, ugonjwa wa pumu. Hili hapa tatizo lingine, shida yako kubwa, wewe si Mkristo, unamhitaji Kristo kuwa Mwokozi wako, maana umetiwa uvuli mweusi. Unamkubali Yesu kama Mwokozi wako? Je, utamkubali kama Mwokozi wako binafsi sasa? Naye atakuponya, na kukupa afya. Utampokea? Mwinulie mkono, useme, “Bwana, ninakuamini.” Kama utafanya hivyo sasa hivi, na kwa moyo wako wote, Yeye atakuponya pumu yako. Uamuzi ni wako.

²⁴⁹ Njoo hapa, uketi chini, uliwazie kwa dakika moja tu. Amini kwa... Unamkubali? [Ndugu huyo anasema, “Naam, ninamkubali.”—Mh.] Basi ninatangaza kwamba umeponywa, katika Jina la Yesu Kristo. Nenda, ukabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, ukiliitia Jina la Bwana.

Unaamini?

Unaamini Yeye atakuponya huo wasiwasi? Vema, endelea, uponywe.

Njoo. Unaamini Yeye atakuponya hicho kisukari? Nenda, ukaponywe, upate afya.

Unaamini yabisi kavu yako itakwisha, na Mungu atakuponya? Nenda, ukaponywe, katika Jina la Bwana.

Unaamini Mungu ataiponya kansa hiyo? Nenda, ukaponywe, katika Jina la Bwana.

Unaamini Yeye ataiponya hiyo kansa na kukupa afya? Nenda, amini, katika Jina la Bwana, na uponywe.

²⁵⁰ “Kama unaweza kuamini!” Unaamini kwa moyo wako wote kila mtu? Kila mtu anaamini? Vipi kama sitakwambia neno, na kukuwekea tu mikono yangu, utapona? Weka... Katika Jina la Yesu Kristo, nenda, ukaponywe. Amina. Amini.

Unaamini kwa moyo wako wote?

²⁵¹ Unaona, tayari umeponywa, wakati mtu huyo huko nyuma alipoponywa ugonjwa huo wa rektamu, kitu kama fistula. Nenda, amini, Bw. Allen, uponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

Njoo. Una ugonjwa wa tumbo, ama ulikuwa nao, nenda, ukale. Yesu Kristo ameninii... .

Unaamini sasa? Kila mtu awe na imani, amini kwa moyo wako wote.

²⁵² Katika Jina la Bwana Yesu, nenda, ukaponywe. Ulisema ulinijua huko nje, na hiyo ndiyo sababu sikusema lolote. Unaweza kwenda. Nenda, ukiwa na imani.

Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe. Amina.

“Ishara hizi zitaifuatana na hao ambao . . .”

Mungu ataponya ugonjwa wako wa figo, kipenzi, utapona, katika Jina la Yesu. Nenda, ukiamini kwa moyo wako wote.

²⁵³ Angalia hapa, mpenzi. Moyo wako utakuwa sawa sasa, nawe utakuwa mzima. Hiyo inakusaidia? Vema, nenda ukaponywe, katika Jina la Yesu.

Ninakibariki kitambaa hiki, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Amini.

Unaamini, dada?

Ninamwomba dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba ataponywa kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Njoo, unahitaji damu, anemia. Unaamini ya kwamba Mungu atakupua ninii . . .

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uupokee. Amina.

Mwaminini Mungu.

Unaamini, bwana?

Katika Jina la Yesu Kristo Mungu wa Mbinguni na akupe afya. Amina.

Iweni na imani sasa, msiwe na shaka.

Ndugu Babbs, njoo hapa. Umekuwa ndugu yangu kwa siku nyingi.

²⁵⁴ Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, tuma baraka Zako juu ya huyu, rafiki yangu mwaminifu, na umpe afya, kwa Jina la Yesu Kristo, ninambariki. Wewe Ambaye ungeweza kuweka tunda katika tumbo la uzazi la binti yake, na kumpa watoto wake wa kupendeza, unaweza pia kuweka uponyaji mwilini mwake. Katika Jina la Yesu, tujalie. Amina.

Rudi, na uwe mzima, ndugu yangu. Mungu akubariki.

Dada Moore, bila shaka, ninakujua, pia.

²⁵⁵ Ee Mungu wa Milele na Mwenye Haki, Muumba wa Mbingu na nchi, mpe baraka Zako huyu, dada yangu. Anaingia kazini Mwako, hivi karibuni, Bwana, ninaamini ya kwamba yeye na Ndugu Jack watakuwa huko nje kazini Mwako kabisa. Sasa ninaomba kwamba huo udhaifu na kadhalika uondoke mwilini mwake, naye aponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, Dada Moore. Nenda, ukiamini sasa. Kweli ninaamini hilo.

“Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana.” Unaamini hilo?

Una wasiwasi, sivyo? Um-hum. Unafikiri sikio lake litakuwa sawa, atakuwa sawa? Vema, nenda ukiamini. Amini.

²⁵⁶ Ee Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utambariki dada yetu. Mponye, ninaomba katika Jina la Yesu, pamoja na kanisa hili kuu, lenye nguvu linaloketi hapa chini ya upako wa Roho Mtakatifu, likiona ishara alizofanya Sulemani, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani, Bwana Yesu Mwenyewe katika umbo la Roho Mtakatifu. Jalia watu hawa wasiwe na shaka kamwe. Ninaomba, katika Jina la Kristo. Amina.

Amini sasa.

Mama.

²⁵⁷ Katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu, ninaweka mikono juu ya huyu mtoto mdogo, na kumkemea ibilisi huyu katika, Jina la Yesu, jalia atoke, na awe mzima. Amina.

Iweni na imani sasa, aminini.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninamkemea ibilisi ambaye amemfanyia dada yangu hivi! Jalia aponywe, katika Jina la Yesu. Amina.

Njoo, dada.

²⁵⁸ Baba Mungu, pamoja na upako Wako hapa juu yetu, na kama Kanisa la Mungu lililokombolewa, tunaomba maombi haya ya imani kwa ajili ya dada yetu, amuru ibilisi huyu amwache, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu wa Milele, Yehova, njoo katika nguvu za kufufuka Kwako na umponye huyu, dada yetu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ee Mungu wa Milele, ondoa wasiwasi kutoka kwa maskini mwanamke huyu, na umruhusu aende na awe mzima, katika Jina la Yesu. Amina.

Sababu ya mimi kusema hivyo, ilikuacha papo hapo, unaona. Nenda ukiamini sasa, na itakuwa sawa.

Baba mbarikiwa, huku mikono imewekwa juu ya mwanamke huyu, pamoja na upako wa Roho Mtakatifu hapa, ninaomba ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu. Amina.

Amini sasa, moyo wako wote.

Yehova Mungu mkuu, ninamwomba dada yangu, pamoja na kanisa hili lenye nguvu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Bwana, huku mikono yangu imewekwa juu ya yake, ninaomba dua hii na maombi haya kwa ajili yake, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Mungu wa Milele, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, Mpaji wa kila karama njema, tuma baraka Zako juu ya dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Baba, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba ya kwamba utamponya mwanamke huyu na kumfanya mzima kabisa, kwa ufufuo wa Kristo. Amina.

Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, mponye msichana huyu mdogo na umfanye mzima kabisa kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

Mungu wa Milele na Mwenye Haki, tunangojea kuuona mkono Wako mkuu. Jongea Ee Mungu, na umponye dada yetu, katika Jina la Yesu.

Mungu wa Milele, Mwanzilishi wa Uzima, mbariki ndugu yangu, ambaye ninambariki katika Jina la Yesu, kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Yehova-Yire, Mponya, njoo na umrehemu maskini mwanamke huyu, mahututi. Jalia aponywe, katika Jina la Yesu. Amina.

Usijali sasa.

²⁵⁹ Yehova Mungu, katika Jina la Yesu Kristo mponye huyu, dada yangu, ambaye ninamwombea. “Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule.” Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Uliahidi jambo hilo, Mungu, ninaliamini, nami ninajua ya kwamba tumetiwa mafuta sasa na Roho Mtakatifu. Amina.

²⁶⁰ Mungu wa Milele, mbariki Dada yangu Schrader, nami ninaomba, Mungu, ya kwamba utampa nguvu ambazo hajawahi kuwa nazo hapo awali. Jalia aondoke hapa, usiku wa leo, katika nguvu na Roho ya Roho Mtakatifu, na akutumikie Wewe siku zote za maisha yake. Pokea utukufu kutoka kwake, Bwana, bali inampasa kuwa na nguvu, mtie nguvu, Bwana. Na huu wasiwasi unaomfanyia uovu huu, ninauhukumu, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁶¹ Dada Schrader, katika Jina la Bwana, huna shida yoyote ila mishipa yako, ninasema hayo katika Jina la Yesu. Huna hata chembe moja ya TB, wala chochote, ni mishipa yako, nayo inakudhoofisha. Kemea kitu hiki, kisha uondoke, na uwe mzima.

Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba ya kwamba utamponya. Katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu wa Milele, ninaweka mikono juu ya huyu, ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Ubarikiwe, ndugu.

Bwana Mungu, Mungu wa majeshi, ninaomba ya kwamba utamsaidia maskini mwanamke huyu mnyonge, na kumpa nguvu, na kumponya, katika Jina la Yesu. Amina.

Nenda ukiwa na furaha, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya mtu huyu, na kumponya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu na kumpa afya, kwa utukufu wa Mungu. Amina.

Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya dada yangu na kumponya. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aende na apate afya. Amina.

Mungu mpendwa, ninaweka mikono yangu juu ya mvulana huyu mdogo na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aende na awe mzima.

²⁶² Mungu wa Mbinguni, ninaweka mikono yangu juu ya dada yangu na kuomba kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba imani yake haitashindwa, ataponywa. Katika Jina la Yesu. Amina.

²⁶³ Mungu, maskini mama huyu aliyeinamisha kichwa chake, ninaomba ya kwamba utamponya. Ninatoa maombi haya ya imani, moyo wangu wote, kwa ajili yake. Katika Jina la Yesu, jalia aende akaponywe.

Ee Mungu wa Milele na Mbarikiwa, ninaweka mikono yangu juu yake, katika Jina la Yesu Kristo, na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Mungu wa Milele na Mbarikiwa, ninaweka mikono yangu juu ya dada yangu na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁶⁴ Baba wa Milele na Mbarikiwa, aliyemfufua Yesu tena katika wafu, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁶⁵ [Ndugu mmoja anasema, “Tuna dada aliyeketi pale, asingeweza kuja, pale amevaa koti jekundu.”—Mh.] Ati mama fulani asingeweza kuja? Moja ya kadi? Yuko wapi, yule ambaye hangeweza kuja, aliyevaa koti jekundu? Ni mama huyu aliyeketi papa hapa? Vema, nitakuja nikuwekee mikono kama unaamini. Hawa hapa, pia.

Je, una kadi? Papa hapa? Naam. Huna? Ugonjwa wa figo ulikuacha, kwa vyovyote vile, kwa hiyo amini tu kwa moyo wako wote.

²⁶⁶ Huh! Ajabu, ugonjwa wa figo, pia. Unaona huyo ibilisi akijaribu kuingia kati ya hao wanawake wawili pale, wakati uo huo tu? Mmoja alimwonya mwingine. Mara tu nilipokutaja,

alienda moja kwa moja kwa yule mwanamke pale, akaja huku na huko, nami nikaona huo mchirizi mweusi ukielekea kule, ndipo nikaona shida yake ilikuwa ni nini, akarudi moja kwa moja, nawe una kitu kile kile. Kusema kweli, una nusu figo tu, lako la kushoto limekwisha, lako la kulia ni nusu tu. Hiyo ni kweli. Unataka kurudi kusini kutoka hapa, na uende salama? Unataka. Utafanya hivyo? Vema, Bi. Dobbs, unaweza kurudi nyumbani ukaponywe basi, kama unaamini kwa moyo wako wote.

Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ninaweka mikono juu ya ndugu yangu, nikiombea uponyaji wake, kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu.

Mungu wa Milele na Mwenye Haki, juu ya kichwa cha dada yangu ninaweka mikono yangu, na kuombea uponyaji wake katika Jina la Yesu.

Mungu mwenye rehema na Mwenyezi . . . 

60-1127E Malkia Wa Kusini
Life Tabernacle
Shreveport, Louisiana Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org